MASWALI NA MAJIBU

Habari za jioni, marafiki, ni vema kuwa hapa usiku huu. Nami . . . jinsi hii ilivyoniangukia, ilikuwa kwa sababu nina . . . nilikuwia nikiwazia asubuhi hii kuhusu ndugu yangu, na kwa sababu najua ibada mbili kwa siku ni nini.

2 Nami ni—nilikuwa na 'siii' kooni mwangu. Nahubiri sana. Halafu mara tu niingiapo mjini, bonde hili, kaa ndogo la kinywa nyuma hapo toka kwa . . . hili, wanaliita . . . Hali hii ya hewa humu bondeni, hulivimbisha vibaya sana yanipasa tu kumezameza wakati wote niwapo hapa hondeni. Nami ninapoondoka, muda wa siku kadhaa, kumekwisha. Kunarudi, kunarudi tena.

3 Nami nilikuwa namhurumia Ndugu Neville, nikijua kuwa—kuwa labda tuko mbele kidogo safarini kuliko vile baadhi yenu watu wadogo mlivyo, na kwa hivyo tunatazama ng'ambo ya pili. Kwa hivyo tunahurumiana sisi kwa sisi, na zaidi sana siku zinapozidi kukaribia, nyakati za maovu zinapokaribia. Huku tukijua kuwa tunaondoka sasa, moja kwa moja, Bwana akipenda.

4 Nami niliwaza, mwajua Ndugu Boze atakuwa hapa Jumapili ijayo jioni, naamini. Mimi . . . Je, mlifahamu hayo? Naam, na Jumapili ijayo jioni. Yeye ana sinema anayotaka kuonyesha, kuhusu kazi za kimishenari katika nchi za ng'ambo ambapo . . . Yeye alikuwa na ndo—ndoto iliyomjia miaka mingi iliyopita, kuhusu kuja Chicago. Na maskini mtu yule alijisikia amevujika moyo wakati mmoja, kasema ujumbe wake haukuwa umetimizwa kamwe. Nami nikamweleza jinsi Bwana alikuwa ameshautimiza. Ndipo yeye akafahamu.

5 Kwa hivyo basi Bwana alimpa ndoto nyingine. Basi tafsiri ilipokuja, ilimwambia aende wapi na afanye nini. Naye akaenda kule na, lo, jamani, kule Kenya na Tanganyika na Uganda, na mataifa yale kule, ni ajabu mno yale Bwana amewafanyia wao katika misheni zao. Naye ataka kuonyesha picha, kuonyesha tu yale Bwana anafanya miongoni mwa watu hao, makabila ya Afrika ndani mle. Bwana akipenda, mnamo Januari, nataka kuungana naye ajili ya . . . na wao miongoni mwa makabila hayo, kwa mkutano kabla sijashuka kwenda Rhodesia na Afrika Kusini tena.

6 Na, ndipo, hiyo ni Jumapili hii ijayo usiku, kwa hivyo kumbukeni, sasa. Basi mwombeeni sana Ndugu Joseph, yeye amekuwa maskini ndugu mzuri. Amenipendeza sana, ushirika wake na mengineyo.

7 Halafu, hili juma lijalo, tunaondoka basi ku . . . kuenda katika Pine ya Kusini, kisha kule Columbia, Carolina ya Kusini;

halafu toka kule hadi Cow Palace, ile Pwani ya Magharibi, ndipo huko Grass Valley; kisha kule kwenye Maonyesho ya Duniani, hatimaye turudi Oregon tena; ndiposa kule British Columbia, na kwingineko, na kuendelea na kuendelea hadi mwisho wa mwaka huu. Ndipo twatumaini, mwishoni mwa mwaka huu, Bwana akipenda, kuwa na mikutano mingine zaidi hapa, Bwana akipenda.

8 Ndiposa nikawazia, kabla sijaondoka, ingekuwa bora kuuliza maswali machache. Mwajua, unaona kile kilicho kwenye mioyo ya watu unapouliza maswali. Na kwa hivyo basi nilidhani, mwajua, usiku huu, kuwa na maongeo ya moyo kwa moyo na hili—hili kundi ndogo, la watu hapa, ku—kuongea nanyi kwa—kwa mioyo yetu. Wakati mwingine nadhani kuwa hilo hufaidi zaidi ya kuhubiri mahubiri, kujaribu tu kufahamikiana sisi vyema zaidi.

9 Tunamshukuru Mungu kwa yale tumeona Yeye akifanya juma hili katika kujibu maombi, imekuwa ya ajabu mno. Na kwa hivyo tuna shukrani, shukrani sana.

10 Nasi twaona majira na wakati wa mwisho vikikaribia, tukijua kuwa kitu fulani karibu kutendeka. Na hakuna ye yote ila yule ajuaye hilo ni kweli, kama yeye—kama yeye ni mtu anayewaza. Twajua, tunatazama hayo katika nyakati zote, kila mmoja ameyatazama. Lakini, mwajua mambo mengi sana yanatendeka sasa. Sisi—sisi twajua hilo ni kweli, haiwezi kuwa mbali sana. Basi huenda nikazungumzia baadhi ya hayo katika dakika chache.

11 Lakini hebu sasa, ili tuanze, tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi. Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nashangaa kama kuna jambo fulani mioyoni mwetu, ambalo tungependa kukumbukwa katika ombi mbele za Mungu. Kama lipo, inua tu mkono wako. Yeye atafahamu, Yeye ajua yote kuhusu hilo. Haja fulani tu ambayo ungetaka kusema, "Mungu, nikumbuke." Bwana awabariki kila mmoja wenu.

12 Baba yetu aliye Mbinguni, usiku huu tunapokaribia hicho Kiti cha Enzi cha neema, ambacho Wewe umetuagiza kwa neema Yako tuje kwa ujasiri mbele za kile Kiti cha Enzi cha Mungu na kwa neema Yake, kuomba dua yo yote ambayo tungehitaji. Wewe ulitwambia sisi kuomba kama tungekuwa na wingi wa watu wawili watatu tukikusanyika pamoja na kukutanika katika Jina Lako, kuwa Wewe ungekuwa kati yetu. Ndiposa cho chote tutakacho, kama tuliomba, yatupasa kupokea tukiamini tu kuwa tungepokea.

13 Wewe wajua hali za nyakati hizi na hali za kanisa na za watu, na za maombi yetu mbele Zako. Sasa, umeshaona hiyo mikono, Bwana. Wajua mioyo ya watu, na hamu zao na mahitaji yao. Nasi twaona wakati unakaribia, yanakusanyika sasa, yale mawingu makuu na yanashuka. Mambo ambayo manabii walinena miaka

mia kadha iliyopita, twaona hayakutendeka hata wakati huu, na ndiyo haya hapa tunayaona moja kwa moja katika siku zetu.

14 Sasa twaomba, Baba, kuwa wewe utatupea baraka hizi tunazoomba waponye wagonjwa na wanaougua. Rudisha katika kanisa Lako, Bwana, nguvu hai za Roho Mtakatifu, imani hai ili kwamba yale tunayoombea tunaamini. Twaamini kuwa sisi tunayapokea kwa sababu tuna hakika itakuwa mapenzi ya Mungu kutupea kabla hatujaomba. Sisi hatuombi bure tunaomba kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kwa hivyo twaomba kuwa utatujalia.

15 Bariki kukusanyika kwetu pamoja, mchungaji wetu, wafanyi kazi wa kanisa, kila mtu, washiriki wa Mwili ule wa Kristo walio hapa. Wale ambao si washiriki wa mwili wa Kristo, wanaotafuta leo mahali pa kujisetiri, wakinunua, kibanda cha kujikinga na bomu nyuma ya nyumba zao, Mungu, na wao waje chini ya kinga ya Bwana Yesu, wakijua kuwa maisha haya yatakapokwisha kuna Uzima baada ya haya. Asante kwa ajili ya ahadi ile.

16 Tupee sisi majibu ya maswali haya usiku huu, ili tuweze kuridhisha kila moyo kwa Neno Lako. Maana twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

17 Tunapokaribia kule kuja kwa Bwana, ni hakikisho kuu jinsi gani!

18 Nilikuwa naongea muda mchache uliopita, mtu fulani alisema jambo fulani kuhusu *bima*, nilikuwa na Wafanyi Biashara Wakristo si muda mrefu umepita katika mojawapo wa mikutano yao, mkutano wa kimataifa. Nilihudhuria tu mmoja, wa jimbo. Mimi hunena kwa niaba ya Wafanyi Bishara wa Injili Nzima, ulimwenguni kote. Na ndiposa kwa kuwa huu—huu mkutano uko Pwani ya Magharibi, huku watu maarufu wameketi pale toka ulimwenguni kote, na . . . wamevalia vilivyo na ni watu waheshimiwa. Mmoja wao aliniambia, "Nilisikia mtu fulani akikuita wewe "Padre."

Nikasema, "Naam, bwana."

Kasema, "Wewe ni mhubiri?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Unafanya nini na wafanyi biashara hawa?"

Nikasema, "Mi—mimi ni mfanyi biashara."

"Ee?" Kasema, "Unafanya biashara ya aina gani."

Nilisema, "Assurance" (Dhamana).

19 Yeye alikosa kufahamu, alidhani nilimaanisha insurance (bima). Kwa hivyo yeye akaniuliza, kasema, "Uko na kampuni gani?"

Nikasema, "Kumpuni ya Kimbinguni."

Akasema, "Sidhani naijua hiyo."

Nikasema—kasema, "Unauza bima aina ga—gani?"

20 "Sikuse-. . ." Nikasema, "Sikusema 'bima', nilisema 'dhamana'."

Kasema, "Unamaana gani?"

Nikasema:

Ndiyo dhamana, Yesu wangu;
Hunipa furaha za Mbingu;
Mrithi wa wokovu wake
Nimezawa kwa Roho Wake.

21 Kwa hivyo, usiku huo nilipokuwa nikijulishwa kwa televisheni, nikasema hayo. Nami nilisema, "Sasa, ni—nina hati za dhamana hapa kama mtu ye yote kati yenu hapa au kote nchini, anayetaka hati za dhamana, ningetaka kuongea nanyi, mara baada ya ibada. Dhamana, ndiyo dhamana!"

22 Sasa, niliwaza, katika kuuliza maswali haya, kuwa huenda nikapata fununu ndogo ya mawazo ye—yenu. Nina mawili. Nilipokuwa nikiingia mlangoni Billy alisema kulikuwa na mengine zaidi, lakini, hakika, sikupata nafasi ya kuyachunguza. Nami nataka kuwa na hakika kuwa ni sahihi Kimaandiko kabla kuyajibu, kwa sababu mlikuwa . . . mnataka iwe hivyo, au kabla sijayajibu. Kwa hivyo labda naweza kuyaweka hayo kwa wakati mwingine. Sasa, moja ya . . . Na katika kujibu maswali haya sasa, kumbukeni, nafanya tu bora niwezavyo.

23 Sijibu maswali katika ibada. Nilijaribu wakati mmoja nami nikaingia shidani. Walikosa kunifahamu. Ilikuwa juu ya Bw. Allen, au kuhusu ishara ya damu na mafuta na kadhalika, mikononi na usoni, kuwa ishara ya Roho Mtakatifu. Nilisema, "Vema, sijui kuhusu hayo," nilisema, "sijaona lo lote la hayo katika Maandiko." Nilisema, "Lakini ni—ninaamini kuwa ninge . . . ningehubiri hivi, ndugu, singeiweka juu ya mwamsho. Nahubiri tu Injili," na nikaendelea.

24 Na kwa hivyo wao walipata barua, kimataifa, "Mpendwa Ndugu Branham . . ." kwa hivyo ilienda kila mahali. Nao walikosa tu kulifahamu. Nasi tuliwatumia kanda na kuwaacha wazisikize tena na kuona ni-. . . Kasema kuwa "nilimhukumu mtu yule." Si—sikufanya hivyo. Sikumhukumu kamwe ndugu ye yote. Wakati mwingine naweza kutokubaliana nao, lakini hilo ni kwa msimamo wa kirafiki.

25 Ndiposa hapa si muda mrefu uliopita mtu fulani aliandika kitabu kuhusu mtu huyu, kuhusu, *Kukamatisha Pepo*. Ndipo niliwazia ingekuwa labda wakati wa kulipia au kumjulisha. Na mtu yule aliyeandika kitabu kile alikuwa ameshutumu kila mwinjilisti hudumani ila mimi, naye alikuwa ameketi papa hapa mkutanoni mwangu, kwa hivyo nilisema, "Sipendelei . . . shutuma hizo, ila . . ." Nilisema . . . Ndugu yule, kwa kweli yeye alitoa sifa hizo kwenye *Christian Digest,* yeye alisema kuwa

mimi ndimi tu sichukui sadaka kamwe na kuombaomba watu pesa, na mengineyo kama hayo, naye alipendelea hilo. Na mtu yule akiketi pale. Lakini kwa bahati nilijua kuwa mtu yule alikuwa amesema kitu fulani kuhusu Ndugu Allen ambacho hakikuwa sahihi.

Yeye alisema, "A.A. Allen alikiandika kitabu hiki cha *Kukamatisha Pepo*."

26 Sasa, A. A. Allen hakuandika kamwe kitabu hicho. Namjua mwandishi wa kitabu hicho. Nami nilisema, "Sasa, kama mtu yule aliyeandika hakuwa mwaminifu kutosha kuenda na kuchunguza ajue ni nani aliyeandika kabla yeye kumshutumu Ndugu Allen, ninaamini ya kwamba baadhi ya shutumu zake zingine haziwapasi ndugu hawa." Ona? Na mtu yule akiketi papo hapo akiniunga mkono. Lakini ilikuwa tu kumjulisha kuwa matamshi yake hayakuwa sahihi, mwaona, kuwa Ndugu Allen hakuandika kitabu hicho, kuandika *Kukamatisha Pepo*.

27 Sasa, katika kujibu maswali haya, yote ni kadiri nijuavyo. Na kama . . . Nitajaribu kuyajibu kwa Maandiko.

28 Sasa, la kwanza lapatikana, naamini, katika I Wakorintho, sura ya 7 na kifungu cha 15. Kwa hivyo sasa tutajaribu kusoma Andiko hilo na kuona lilivyo, na kuona kama tunaweza kumsaidia huyu ndugu mpendwa anayeuliza swali hili. Sasa, I Wakorintho, sura ya 7, kifungu cha 15. Nadhani mtu yule ako humu sasa. Basi linasema hivi:

> *Lakini yule* asiyeolewa *akaondoka, na aondoke. Hapo huyo ndugu mume au ndugu mke hafungiki. Lakini Mungu ametuita katika amani.*

169. Sasa, I Wakorintho, sura ya 7, kifungu cha 15. Sasa swali walilouliza; **Ndugu Branham, je, hii yaonyesha kuwa ndugu mke au ndugu mume yu huru kuoana au kuolewa tena?** La.

29 Ona, hupati swali lake hapo na yale anayosema. Hawako huru. Ona, hilo lingefarakanisha Maandiko, na Maandiko hayahitilafiani kwa vyo vyote vile. Ona? Sasa, hebu . . . Mwaona, kama unavyoweza kufanya Maandiko (kwa kusoma tu kifungu kimoja) yaseme lo lote unalotaka yaseme, kutosheleza nia yako. Lakini yakupasa uchukue lile wazo yanalonena juu yake.

30 Kama—kama nilikuwa naongea na Ndugu Neville nawe nawe ukanisikia nikisema neno "board".

31 Basi ungaliondoka, useme, "Mwajua anayonena? Tulimchosha (bored) usiku huu." Ona? "La", mtu yule mwingine angesema, "si hivyo, ilimaanisha kuwa yeye—yeye anawiwa na board (halmashauri), yeye alikuwa akilipa." Mwingine asema, "Ee, la, yeye hakukusudia hilo, yeye alimaanisha board (ubao) kwenye kuta za nyumba." Na mwingine aseme, "La, hebu niwaambieni, naamini yeye alikuwa akijaribu kuongea juu ya boring (kuchimba) shimo." Ona? Ona?

32 Yakupasa upate maongezi yale, ndipo ujue yale unayonena, kwa sababu Paulo hapa wakati mwingine anajibu maswali yao.

33 Wakati mwingine wao husema, "Biblia inahitilafiana." Nataka kupata hilo. Haihitalifiani. Mimi—mimi nina miaka thelathini na miwili mimbarani, sijawahi kuona hitilafu bado. Ona? Haihitilafiani! Iko. . . Wewe ndiwe unayeipinga, ona, na huifahamu. Roho Mtakatifu ni Mfunusi, Mfunuaji wa Neno. Kwa hivyo, kuhitilafiana kule. . .

34 Ona, Paulo anawaandikia watu wale, akisema, "Mliuliza jambo *fulani na fulani"*. Isipokuwa, yeye hasemi tu ya kwamba mliuliza, yeye *ananena* tu hayo. Ndipo hapa yeye anageuka na kuyajibu tena, bali hailingani na yale waliyouliza.

35 Wao waliuliza, "Si tunafanya *hiki,* na *hiki* na *hiki."* Na Paulo ageuka na asema jambo lingine ona, inaonekana kama ni kuhitilafiana. Sivyo. Kama ungesoma tu kifungu chote, sura yote, ungetambua kuwa yeye ana—yeye anajaribu kueleza yale wao wamemwandikia.

36 Sasa, papa hapa hilo lingeonekana kama lingetoa. . . Na hivyo ndivyo upatapo tatanisho katika Biblia, lakini sivyo ilivyo. Sasa, inaonekana kama, hapa, mtu huyo anataka kujua, au swali wanalotaka kujua:

> **Je, ndugu au ndugu mke katika Bwana, aweza kuoa au kuolewa tena na kuwa huru, wakiachana na wenzao na kuoa au kuolewa tena?** La.

37 Sasa hebu tuchukue. . . tuanzie kifungu cha 10:

> . . .*wale waliokwisha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila Bwana,* (Ona?) *mke asiachane na mumewe;* (Ona?)
>
> *Lakini. . . ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, au apatane na mumewe; tena mume asimwache mkewe.* (Hiyo ni Amri ya Bwana, ona)
>
> *Lakini watu wengine nawaambia mimi, wala si Bwana;* (Ona?) *ya kwamba iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini,. . .*

38 Sasa, chunguza somo hili, ona. Na uendelee kusoma chini kabla ya haya, usome sura hii yote, utaona kuwa wao walidhani, "Kama tulimwoa mke naye alikuwa. . . sisi. . . nilioa kisha nikawa mwamini, na mke wangu hakuwa mwamini, hebu nimwache." Jamani, la. Hilo sivyo. Huwezi kufanya hilo. Ona? Ona;

> . . .*iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini, na mke huyo anakubali kukaa naye, asimwache.* (Yaani, si kwa sababu ya ndoa, hiyo ni kwa sababu ya kutokuamini. Si "kuoa tena." Ona. Kaa naye!).

Na mwanamke, ambaye ana mume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye, asimwache mumewe. (Naam! Ona?)

Kwa maana yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe; na yule mke asiyeamini hutakaswa katika mumewe; kama isingekuwa hivyo, watoto wenu wangekuwa si safi; bali sasa ni watakatifu.

Lakini yule asiyeamini akiondoka, na aondoke . . .

39 Sasa, yule asiyeamini akisema, "Sitaishi nawe tena, wewe umekuwa Mkristo." Ku . . . Mwanamume amwambie mkewe, "Kwa sababu umeokoka, na umeondoka ulimwenguni ambapo tulikuwa, nitakuacha." Sasa, hakuna cho chote uwezacho kufanya kuhusu hayo, mwache aende. Ona?

40 Au mwanamke amwambie mumewe, "Siendi kujichanganyisha na hilo kundi la watakatifu wanaojigaragaza. Sitafanya hili! Nitajitenga na kuachana nawe." Usiondoke kanisani, mwache huyo mwanamke aondoke. Ona?

41 Ndugu au dada hafungiki katika hali kama hiyo, yaani, kama mwenzio anakuacha na ataka kuondoka kwa ajili ya Hilo. Haikupasi kujishikilia kwao. Kama wanataka kuachana nawe na wanakuacha kwa ajili ya Kristo, acha waende. Lakini hauwezi kuoa au kuolewa tena. "Lakini Mungu ametuita katika amani." Ona? Sasa. Si kwamba unaweza kuoa au kuolewa tena, yeye amekwisha eleza hayo, lakini si lazima kuishi na mume asiyeamini au mke asiyeamini kama hawataki.

42 Kama wanataka, kasema, "Sasa, wewe nenda kanisani. Na ukitaka kuenda kule, hiyo ni juu yako. Ukitaka kuhudhuria kanisa lako, endelea. Kwangu, siamini Hilo. Na ni—nitakufanyia wewe lo lote, sitakuzuia, endelea. Kwangu mimi, siamini Hilo. Ni—nitakupa msaada wo wote, sitakuzuia, endelea tu," ndipo baki tu pale, bila kujua kwamba maisha yako yaliyotakasika yatamtakasa mwamini huyo, kuwafanya waamini. Ona? Upande wo wote, mwanamume au mwanamke, ona. Mna . . .

43 Lakini sasa kusema tu, "Mimi . . . Ndugu Branham, nilioa na mke wangu si mwamini, na hapa kuna dada humu ninayeweza kumwoa. Nitamwacha huyu na kumwoa huyo." Jamani, la! La, hakika! Nadhiri yako ni hata kifo kitakapowatenganisha, na hakuna kingine ulimwenguni kitakachokuruhusu kuoa (katika Biblia) hadi mwenzio atakapokufa. Naam. Hiyo ndiyo sababu pekee! Hakuna kuoa au kuolewa tena po pote kamwe, isipokuwa mwenzio amekufa. Hivyo tu. Ona?

44 Huwezi kulifanya lihitilafiane. Kwa hivyo soma tu vifungu vile vilivyotangulia na vifuatavyo, na utashika basi yale yeye anayonena. Sasa, hili hapa lamaanisha, si . . . Ona:

Je, hii inamaanisha ndugu mke au ndugu mume yu huru kuoa au kuolewa tena?

45 La, bwana. Ona, yeye alilieleza hilo kwanza. Ona:

> . . . *wale waliokwisha kuoana nawaagiza, wala hapo si mimi, ila Bwana; mke asiachane na mumewe;*
>
> *Lakini, ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, au apatane na mumewe;* . . . (Ona?)

46 Hakuna kitu kama mwamini ye yote kupatanishwa apate kuoa au kuolewa tena kamwe, iwapo ana mwenziwe aliye hai.

Sasa, hapa kuna lingine. La pili liko hivi:

170. Waovu watakuwa na mwili wa namna gani katika ufufuo wa mwisho wa ile Hukumu ya kile Kiti Cha Enzi, Kikubwa, Cheupe?

47 Mwenye dhambi huyo atafufuka katika ule ufufuo akahukumiwe katika mwili ule ambao alitendea dhambi. Ona? Itampasa yeye kusimama Hukumuni katika ufufuo.

48 *Kufufuka* si kubadilishwa, ni "kurudisha tena kile kilichoenda chini." Yesu alipofufuka toka kwa wafu, Yeye alikuwa na mwili ule ule uliozikiwa, Yeye alifufuka katika namna ile ile ya mwili. Sisi tutafufuka katika mwili ule ule tunaoenda chini nao, ni ufufuo, si badilisho.

49 Sasa, Biblia yasema kuwa ile . . . ya kwamba tutahukumiwa kulingana na dhambi zilizotendwa katika mwili. Na, mwovu atakapofufuliwa, atahukumiwa katika mwili ule ule aliotendea dhambi, kitu kile kile.

171. "Adamu akamjua Hawa mkewe; naye" (kiunganisho) "naye akapata mimba, akamzaa Kaini." Naamini yote unayofundisha, ila nime- . . . ninge- . . . Ningemjibu namna gani mtu anaye—anayesema Hawa hakupata mimba baada ya Adamu kumjua, kwa sababu ya kiunganisho kile "naye". "Adamu akamjua mkwewe; naye akapata mimba akamzaa Kaini.

50 Sasa, sisi watu wazima twajua maana ya "akamjua." Sasa, swali ni kuhusu kiunganisho kile. Sasa, kama mtachunguza, marafiki, ona, hamwe—hamwezi kufanya Biblia iseme kitu kimoja mahali pamoja na kitu kingine mahali pengine. Haina budi kusema kitu kile kile wakati wote. Na kama unaifanya iseme jambo moja hapa na jambo lingine humu, basi tafsiri yako si sahihi. Ona? Huwezi kufanya vile. Huwezi kumpata Hawa amedanganywa na shetani kisha umpate mahali pengine amedanganywa tena. Ona? Na mara ya kwanza yeye alipodanganywa alipopata mimba. Huwezi kumfanya yeye adanganywe mara mbili.

51 Hebu niwaelezeni habari za viunganisho vyenu. Katika kusoma Biblia yapasa ujue ambapo viunganisho vyako vinawekwa. *Kiunganisho* ni cha kuweka fungu lako la maneno pamoja. Ona? Sasa tazama hili. Sasa, katika Mwanzo 1:26, chunguza kiunganisho hiki, ndiposa ukaeleze hili kisha

nitakwaambia jinsi yeye. . . Adamu alipomjua mkewe. Mwanzo, sura ya 1, na kuanzia kifungu cha 26. Sasa, sikizeni kwa makini. Mungu amefanya viumbe Vyake sasa, na Mungu akafanya nchi izae vitu vitambaavyo na vitu vyote ambavyo nchi ilizaa. Sasa, katika mlango wa 26. . . kifungu cha 26 cha ile sura ya Kwanza ya Mwanzo:

> *Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura—kwa sura yetu. . . wakatawale* (mtu). . . (si *akatawale;* "wakatawale," ona, wingi) *wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani na wanyama, na nchi*. . . (Ona ile "na, na, na" zikiyaunganisha pamoja?). . . *na nchi yote pia, na kila chenye kutambaacho juu ya nchi.*
>
> *Mungu akaumba mtu kwa mfano Wake, kwa mfano wa Mungu aliwaumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba* (wote wawili wanamume na mwanamke).
>
> *Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, na* (na) *mkaijaze nchi, na kuitiisha;*

52 Kiunganisho baada ya kiunganisho cha yale. . . Mwanadamu aongezeke. *Na* baada ya kuzaana aongezeke, ndipo akaitiishe nchi; hayo ni mpaka ule Utawala wa Miaka Elfu. Ona? Vema, kuitiisha nchi. Vema:

> *. . . mkatawale samaki wa baharini, na. . . ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi.*

53 Sasa, Mungu alimwumba mtu katika mfano Wake, akamwumba, na wakatawale (mtu yule) nchi, yote, na kuitiisha na kadhalika, na wafanye hili na watawale samaki wa baharini. . . na kila kitu ambacho yeye alifanya. Ndiposa tunaona katika Mwanzo 2:7. . . Sikiza hili. Baada ya Mungu kuifanya nchi, kuumba mtu, kumpa utawala juu ya nchi, akiisha kumpa kila kitu alicho nacho, na Mungu aliwaumba, akawaambia wazaa-. . . Wazae wakaijaze nchi, na mambo haya yote, na baada ya vifungu saba zaidi vya vitu alivyokuwa amemaliza, na mbingu na nchi na kila kitu, "Na Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi." "Na!" Ndiye huyu hapa ("na" *kiunganisho)* akimfanya mtu ambaye Yeye alikuwa amekwisha muumba. Ona? Akamfanya mtu:

> *Na*. . . (kuyaunganisha mafungu Yake ya maneno pamoja). . . *Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia* (pumzi) *puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.*

54 Sasa, waza hilo! Baada ya kumfanya mtu (mwanamke na mwanamume) katika Mwanzo 1:26 hadi 28, Yeye alimfanya mtu kwa mfano Wake, akamwumba na kumpa. . . akazitiisha falme na kumpa mamlaka haya yote na kila kitu, na yeye alikuwa bado hajamwumba mtu.

55 Ona, Shetani alikuwa amekwisha kumdanganya Hawa. Hakika, Adamu alimjua, lakini yeye alikuwa amekwisha danganywa. Kwa sababu nyuma hapa yeye. . . wao walipo-. . . kabla wao hawajakuja. . . Wao walipofika hukumuni, Yeye alisema,. . . Mungu aliwakusanya pamoja na kusema, "Nani alifanya hili?" Aliwauliza swali lile.

Adamu akasema, "Huyo mwanamke uliyenipa."

Na mwanake akasema, "Nyoka alinidanganya."

56 Na Mungu aliweka laana juu yao, na kila kitu hivyo. *Ndiposa* Adamu akamjua mkewe, ona, baada ya kadanganywa na kuwa mama.Kama tu vile Mungu alivyomfanya mtu nyuma hapa katika Mwanzo 1:26 hali yeye hakuwa amefanywa bado. Ona? Vema.

57 Sasa chunguza, hebu tufikie chini hapa na kusoma, pia:

> *Adamu akamwita mkewe jina lake. . . Hawa; kwa kuwa yeye ndiye aliye mama wa viumbe wote walio* hai, wote. . . au *mama yao wote walio hai.* Akamwita mkewe. . . akamwita mwanamke yule mkewe kwa sababu Hawa alikuwa. . . yao wote walio hai.
>
> *BWANA Mungu akamfanyia Adamu na mkewe. . . mavazi ya ngozi, akawavika.*

58 Sasa, sasa chunguza katika Mwanzo tena, 1:21, Mungu aliumba nyangumi wa baharini. Yeye alifanya kila kitu, na kuumba vitu vyote, kumwumba mtu katika mfano Wake. Akamfanya, si mtu "mmoja", mtu mzima, hao wote katika Mfano Wake. Ona? Na katika mfano wa Mungu Yeye akawaumba; mwanamume na mwanamke, akawaumba wote wawili hivyo.

59 Na sasa twaona, hapa tena, baada ya Yeye kumfanya mtu katika mfano Wake, baada ya kumwumba hapa mwanamume na mwanamke, hapa Yeye anamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi.

60 Ndiposa, baada ya kutenda hayo, baada ya kumfanya yeye mwanamume na mwanamke, ndipo Yeye arudi hapa na kumfanyia mwanamke, baada ya kumfanya mwanamume yule. Ona?

61 Ona, kiunganisho chako kinaunganisha fungu hilo la maneno pamoja. Kama tu vile ilivyosema, sasa *hapa*, "Mungu akaumba mtu kwa mfano Wake, na kwa mfano Wake akamwumba," ni Mungu akinena katika mawazo Yake, niani Mwake, aliyokuwa nayo. *Hapa* ndipo Yeye alipofanya tendo lile hasa.

62 Yesu alikuwa yule Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu; yeye hakuchinjwa miaka elfu nne baadaye. Ona?

63 Kwa hivyo yule nyoka alikuwa amemdanganya Hawa. Hilo ni kweli. Ndipo baada ya hukumu kutolewa, basi Adamu akamjua mke wake. Ndiposa akapata mimba akamzaa mwana, Kaini. Mwafahamu? Ona, kiunganisho hicho kinaendeleza tu yale Adamu aliyofanya, si yale yaliyofanywa kabla ya Adamu.

64 Basi tazama hapa, kama ungetaka kuendeleza hayo, katika matamshi hayo makuu hapa, naamini tunayapata hayo juu hapa katika sura ya 4, naamini ndipo.

> *Adamu akamjua. . .mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, na* (kiunganisho) *akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa BWANA.*

65 Basi hakika haikuwa Adamu, ilikuwa mwana wa Mungu kwake. Ona? Ona? Ukitaka kuweka pale kiunganisho chako, ona, ("na" tena), "Nimempata mtoto mwanamume kwa Mungu." Ndipo kusema kuwa Mungu alimpa hicho kiumbe cha ubaguzi kinachoitwa Kaini? Ilitoka wapi hiyo asili ya mambo hayo yote mapotovu na maovu na kadhalika aliyokuwa nayo Kaini, yalitoka kwa Mungu? Hasha! Ona? Yeye alidanganywa na yule nyoka, naye nyoka. . .yeye alikuwa ameshakuwa mama. Ndipo Adamu akamjua, bila shaka alimjua, yeye aliondoka akaishi naye kama mkewe, lakini alikuwa amekwisha kuwa mama wa mtoto huyu.

66 Ndiposa hatimaye mwana wa Adamu alipozaliwa, yeye alikuwa mwenye utu wema, mtu mzuri, mnyenyekevu, mtu mpole kama Adamu.

67 Lakini mtu huyu, huo udanganyifu halisi ulitoka wapi. . . Dhambi ile ilitoka wapi? Mtu huyu, Kaini, huyo muuaji alitoka wapi? Na Biblia ilisema kuwa "Shetani ni muuaji." Uongo huo ulitoka wapi? (Shetani ni baba wa uongo; yeye ni mwongo na baba wa uongo.) Hapana budi ulitoka kwa asilia fulani mbali na Mungu. Kwa hivyo Kaini alikuwa yule mwovu, na baba yake alikuwa Shetani; naye alimzaa huyu mwovu.

Halafu, hakika, Adamu alimjua mkewe, bila shaka.

68 Na, naam, labda kama ungesema hivi. Huenda nikasema, nikijichukua mwenyewe, vema, sasa, Rebeka alizaliwa, na baada ya kitambo kidogo akaja. . .

69 Siku moja nilikuwa nikisoma hadithi ya Yusufu, nami nilifurahishwa sana na hadithi hiyo ya Yusufu. Nikaingia katika chumba kidogo na kupiga magoti, kule Minneapolis, nami nikasema, "Bwana Mungu, jinsi ninavyokushukuru kwa ajili ya mtu kama Yusufu!" Nami nikawazia, "Kama ninge. . .Laiti ningelimwita Billy Paul, 'Yusufu' kama huyo mtu mkuu na mwema sana." Hamna neno dhidi yake po pote katika Biblia, mfano mkamilifu wa Kristo katika kila njia. Kawazia, "Jinsi ningependa. . ." Nilisema, "Ee, ningelimzaa mwana wa kiume, ningemwita 'Yusufu.'"

70 Mara ile Nuru ikaingia katika jengo lile ikasema, “Utapata mtoto wa kiume, nawe utamwita jina lake ‘Yusufu.’”

71 Nikamjua mke wangu, hakika, akamzaa Sara. Ndipo nikamjua mke wangu *na* akamzaa Yusufu. Mwafahamu ninalomaanisha? Ona, haikuhusiana na yule wa kwanza kwa vyo vyote vile. Ahadi ya Mungu ilikuwa “Yusufu,” Sara alikuja kati yake. Si kumweka Sara katika hali mbaya kama hiyo, lakini kuwaonyesha ninyi kile ni—kile ninachokusudia. Ona, hilo . . . Sara alitumwa na Mungu, pia. Na kwa hivyo basi twajua hilo.

72 Sasa, lakini, ona. Mungu, Yeye alipotoa hukumu juu ya Adamu na Hawa, Hawa alikuwa amekwisha tenda dhambi ile kabla Yeye hajatoa ile hukumu. Na, sikizeni, mliwahi kujua kuwa mwana wa kwanza aliyewahi kuzaliwa ulimwenguni “alizaliwa katika dhambi, akaumbika katika maovu, akaja ulimwenguni akinena uongo”? Yule wa kwanza aliyepata kuzaliwa alizaliwa hivyo, kwa sababu . . .

73 “Na adamu na hawa je?” Hawakuzaliwa. Waliumbwa. Ona?

74 Lakini yule mtoto wa kwanza aliyewahi kuja alizaliwa katika dhambi, kwa hivyo haina budi kufuata huo mstari. “Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu.” Yeye amezaliwa katika dhambi. Hiyo ndiyo sababu hana budi kuzaliwa mara ya pili, ona, kwa Roho; si kwa *wazo* la roho; kwa Kuzaliwa na roho, ona, ambayo humzaa upya, humfanya kiumbe kipya. Mtu wa kwanza kuzaliwa alizaliwa katika dhambi.

75 Ndipo, ilipaswa kuweko Mmoja aliyekuja bila kujuana kimwili. Sasa, kama kujuana kimwili hakukuwa tendo la kwanza, basi mbona walipaswa kuwa na Mmoja aliyezaliwa kukomboa uzao wote wa mwanadamu? Mbona Yeye asimlete mmoja kutoka juu kwenye vile ukumbi na kusema, “Hapa kuna Mmoja *anayewaza* sahihi?” Ilipaswa kuja kwa kuzaliwa kimwili, ilikuja kupitia kwa mwanamke, kwa sababu hapo ndipo iliingilia kwanza. Kupitia kwa kujuana kimwili ukaja uovu; na kupitia kwa kujuana kimwili ikaja Haki. Ona? Mungu, bila uasherati, bila tamaa ya kimwili, akamzaa Yesu Kristo kwa uzazi usio na dhambi, kwa kumtilia Mariamu uvuli na kuumba ndani yake mtoto huyu mchanga, aliyekuja kwa kujuana kimwili. Na, kupitia kwa hayo, Damu Yake Takatifu ilikomboa uzao wote ulioanguka wa mwanadamu. Ona? Kwa hivyo lazima iwe vile, hakuna njia nyingine yo yo yote kwa hilo.

76 Kila mtu aliyezaliwa na mwanamke yuaelekea mautini, yeye yu maiti anapozaliwa. Naam.

77 Hiyo ndiyo sababu nilikuwa nikiongea hivi majuzi jinsi tulivyo na hiyo dhamana iliyobarikiwa sasa.

78 Wakati Israeli ilipo . . . si . . . Mimi hunena mambo mengi sana ambayo hayana faida lakini wakati mwigine Bwana hunipa jambo fulani ambalo hunichangamsha. Kwa hivyo

Yeye aliponipa hilo, lilinichangamsha zaidi ya cho chote kile ambacho nimewahi kupata kwa miaka mingi. Yeye aliponipa hilo hivi majuzi, nilipoona kuwa Israeli (mtumwa) hawakuwa na makao, wana wa Mungu. Kapata mikate yenye kutu, cho chote walichotaka kufanya! Ee, laiti wangekuwa na makao ambamo wangeishi kwa amani, wapate riziki zao kwa jasho la nyuso zao!

79 Na, siku moja, akashuka nabii toka jangwani, akiongozwa na Nguzo ya Moto, akawaambia kuhusu nchi ya ahadi. Hakuna ye yote aliyewahi kuwa kule, hawakujua lo lote juu yake. Lakini ilikuwa ahadi. Kwa hivyo wakaamini na kumfuata nabii huyu hata walipokaribia ile nchi ya ahadi.

80 Ndipo kuna shahidi aliyeitwa *Yoshua* ambalo maana yake ni "Yehova-Mwokozi," aliyevuka Yordani akaingia katika ile nchi ya ahadi, na akurudi na ushahidi kuwa nchi hiyo ilikuwa tu hasa jinsi nabii huyo alivyosema ilikuwa kwa Neno la Mungu. Walikuwa na kichala cha zabibu, zilizohitaji watu wawili kubeba, nao wangeonja matunda ya asili toka kwa nchi hiyo. Hakuna ye yote aliyejua nchi hiyo ilikuweko, waliamini tu. Walitoka wakaenda kwa imani na kuiamini.

81 Sasa, waliporithi nchi yao, walikuwa na furaha jinsi gani! Kila mmoja angeishi kwa amani, awe na bustani yake ndogo, awazae watoto wake na kadhalika. Lakini, hata hivyo, uzee baadaye ulimkumba, na mauti ikamnasa na kumtwaa.

82 Ndipo huku akishuka toka kwa ukumbi wa mbinguni, kupitia kwa mwanamke, akaja shujaa mwingine mkuu, zaidi ya hao wote, Mungu Mwenyewe aliyedhihirika katika mwili, Yesu Kristo. Naye akawaambia Israeli jinsi walivyokuwa watu wakuu, lakini walikabiliwa na mauti, Yeye alisema, "Lakini nawaeleza kuhusu nchi nyingine. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Kama sivyo ningaliwaambia. Ninyi mna furaha katika nchi yenu mna makao yenu, mna watoto wenu. Lakini mnamzika kila mmoja wao kule na inaonekana kana kwamba ndio mwisho."

83 Ayubu aliiona, kasema, "Mti ukifa, unaishi tena. Lakini mwanadamu hulala na kutoa roho, naye yupo wapi? Wanawe huja kutoa heshima zao naye hajui. Ee, laiti ungenificha kuzimuni, ukanilinda kwa siri, hata ghadhabu zako zitakapopita!" Yeye alisema, "Mtu akifa je! ataishi tena?"

84 Miaka elfu nne hapo awali, walitazamia kitu fulani ng'ambo ya kaburi hilo. Mambo yote makuu ambayo Mungu aliwapa, makao, jamaa na watoto, na kanisa, na kila kitu, na manabii, na mtu mkuu hata wakati huu, hata hivyo kila mmoja alikufa akaenda kaburini mwake. Lakini hapa yuaja Mmoja na kusema, "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi, nami naenda kuwaandalia makao."

85 Kama Yoshua, yeye alikutana na Kadeshi-barnea yake. Israeli ilipofikia Kadeshi-barnea . . . Na Kadeshi ilikuwa kiti cha

hukumu cha ulimwengu wakati huo, visima saba toka kwa kisima kimoja kikubwa, vikimaanisha hukumu, kama Nyumba ya Mungu na Makanisa yanayotoka kwayo. Naye Yoshua, toka Kadeshi-barnea, alivuka akaingia katika ile nchi ya ahadi kuleta thibitisho.

86 Sasa, Yesu alikutana na *Kadeshi* Yake. Ilikuwa nini? Kiti cha hukumu! Ilikuwa wapi? Kule Kalvari, ambapo Mungu alimhukumu Yeye kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Walifanyaje? Yeye alikabiliana na mauti, ile ghadhabu ya Mungu. Kuwapatanisha wenye dhambi kwa Mungu, Yeye aliona mauti na akavuka ule mto Yordani (wa mauti). Wakamzika.

87 Yeye alikufa hata mwezi na nyota vikaaibika. Yeye alikufa hata dunia ikakumbwa na fadhaa. Ilitetemeka hata miamba ikafingirika toka milimani. Ilitetemeka hata nyota hazingeng'aa, mwezi haungeangaza, nalo jua likatua mchana. Akafa! Alikufa kabisa hata Mrumi akachukua mkuki wa ratili kumi na akamchoma kabisa moyoni Mwake; maji na Damu. Yeye Akakuwa amekufa! Yeye alivuka Yordani. Nao wakamlaza kaburini na kufingirisha ji—jiwe juu Yake, ilichukua karne ya watu kufanya hivyo. Alikuwa amekufa! Waliweka muhuri wa Kirumu juu yake.

88 Lakini asubuhi ya Pasaka Yeye alirudi toka upande wa pili wa Yordani, na kasema, "Mimi ndiye niliyekuwa nimekufa; na naisha tena milele!"

Wengine wao walisema, "Tunaona pepo."

89 Kasema, "Niguse, je, roho ana mwili na mifupa kama nilivyo nayo?" Kasema, "Mna chakula cho chote? Nileteeni kitu fulani." Nao wakampa samaki na mkate. Naye akala. Yeye alikuwa mtu!

90 Alikuwa nini? Kuleta thibitisho kuwa kuna Nchi tunayoiendea. Yeye alifanyaje? Yeye, kama Yoshua, Yeye alileta thibitisho lake. Yeye alisema, "Sasa, mkitaka thibitisho lake, 'Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea Roho Mtakatifu.' Huo ndio ushuhuda ulionifufua mimi. Nitawapa Arabuni ya urithi wenu." Halafu ikawa vipi? Katika siku ya Pentekoste Roho Mtakatifu alikuja juu ya mwamini.

91 Sasa, tunafanyaje? Tunaungama dhambi zetu, tukijihesabu kuwa wafu, tumezikwa pamoja naye katika ubatizo, tukafufuka pamoja Naye katika ufufuo Wake. Kufanyaje? "Kuketi katika ulimwengu wa roho pamoja Naye." Hapo ndipo tulipo usiku huu, tumeketi (si kwa kuonekana) kiroho, nia zetu, mawazo yetu, nafsi zetu ziko mbali sana na shughuli za dunia hivi sasa. Sisi ni nini? "Katika ulimwengu wa roho KATIKA Kristo Yesu." Tunaingiaje ndani Yake? "Kwa roho mmoja," I Wakorintho, sura ya 12, "kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kwa Roho Mtakatifu kuwa Mwili mmoja wa waamini." Ule Ufalme usioonekana wa Mungu!

92 Ndani mle twatazama nyuma na kuona ambapo tulikuwa tukisema uongo na kuiba na kudanganya na kuvuta sigara na kufanya mambo maovu. Tumeinuliwa toka kwa hayo. Tuko katika ulimwengu wa roho. Ni nini? Thibitisho kuwa siku moja tutakuwa na mwili kama Wake Mwenyewe uliotukuzwa. Ni thibitisho hasa la ufufuo kwa sababu, kwa kuwezekana, tumekwisha kufufuliwa pamoja naye, kwa kuwezekana tumekwisha kufa.

93 William Branham aliyekuwa akiisha haishi tena, yeye amekuwa mfu kwa miaka thelathini na kitu, sasa ni kiumbe kipya. Orman Neville aliyekuwa akiishi haishi tena, yeye alikufa miaka mingi iliyopita, hiki ni kiumbe kipya. Orman Neville amekufa, yule—yule saisi wa farasi, mcheza kamari, au vyo vyote alivyokuwa, mtu yule aliyekuwa akiishi wakati mmoja amekufa. Sijui, Ndugu Neville hakuwa hivyo; lakini vyo vyote alivyokuwa, yeye ana hatia ya hayo yote, "Mwenyewe hatia kwa madogo yuna hatia kwa yote." Haidhuru ulikuwa nini, wewe u mwenye dhambi, hivyo ndivyo ulivyo.

94 Nawe u mfu kwa sababu unapenda mambo ya ulimwenguni. Na mradi ungali unapenda ulimwengu, haidhuru unakiri jinsi gani kuwa juu *hapa*, wewe bado haupo juu hapa, wewe bado uko chini *pale*. "Yeye apendaye dunia na mambo yaliyomo katika dunia upendo wa Mungu bado haujamwingia."

95 Lakini unapoinuka juu ya hayo hadi kwa mambo ya Kimbinguni ndipo unayafikiri yaliyo juu, kwa sababu umefufuka pamoja na Kristo na sasa umeketi pamoja naye katika ulimwengu wa roho. Jua kwa yakini, hakuna kiwezacho kukudhuru, hamna hata kimoja. Hata kifo chenyewe hakika . . . hakiwezi kukufanya lo lote. Wewe umekwisha tiwa nanga katika Kristo. Ile dhamana, ile Arubuni, yale malipo ya kwanza yamekwisha letwa, umeyakubali. Ulifanyaje? Umefufuka pamoja Naye katika ufufuo.

96 Tazama kule nyuma nilipokuwa wakati mmoja. Sasa niko juu yake. Mbona? Kwa neema Yake Yeye aliniinua juu, na ndimi huyu hapa nimeketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo. Ee, lo! Naam. Ndipo Biblia inakuwa Kitabu kipya. Ndipo unaisoma kwa macho ya roho na ufahamu wa rohoni. Ndipo unaona majina na vijina, kisha unaona njia panda . . . na viunganisho, na kadhalika, katika Biblia.

97 Ee, ambapo inasema . . . Wao husema, "Inahitilafiana Yenyewe"; uko chini *hapa* ukisoma. Unasimama *hapa* na kuisoma, yote iko tofauti basi. Mwaona? Hiyo ni kweli. Hakika. Hakika, inakuwa kitu kipya kabisa unapoisoma katika roho. Naam.

Hili swali lingine hakika si swali, lasema tu:

172. Niliishi miaka mingi dhambini hata nilipompokea bwana. Tafadhali, Ndugu Branham, nimetenda dhambi tena na

> **sistahili kuja mbele zenu katika mahali hapa patakatifu. Tafadhali niambie kama naweza kurudishwa tena kabisa. Tafadhali nisaidie, Ndugu Branham, nina pepo ndani yangu. Nisaidie! Je, utaweka mikono yako juu yangu na kunirudisha mimi tena?**

98 Sasa, kuna swali, sikuliona kamwe nilipolisoma muda mchache uliopita. Kuna swali. Sasa, kama mtu yule yumo humu . . . Hebu niwasomeeni tu ninyi:

> **Nimeishi—nimeishi miaka mingi dhambini hata nilipompokea Bwana. Tafadhali, Ndugu Branham . . .** (Ona?) **. . . nimetenda dhambi tena na sistahili kuja mbele yenu katika mahali hapa patakatifu. Tafadhali niambie kama naweza kurudishwa tena kabisa.** Naam.

99 Haujatenda dhambi sana (rafiki yangu) kwa Mungu ila kwamba waweza kurudishwa. Kama ulikuwa umetenda dhambi sana hata haungeweza kurudishwa tena *haungalitaka* kurudishwa. Ona? Ona? Lakini mradi kuna kitu fulani kinachoshughulikia moyo wako, wewe bado uko katika njia ya kurudishwa tena.

100 "Mwenye hatia katika madogo sana ana hatia katika yote." Nimetenda dhambi mara nyingi, kila siku kila mmoja wetu hutenda mambo ambayo hatutaki kutenda.

101 Imo ndani ya mioyo yetu . . . Hutaki kuwa hivyo au haungeuliza swali hili. Ona? Hilo lenyewe ni thibitisho kuwa Mungu bado anakushughulikia wewe. (Huenda wewe umeshikwa na wasiwasi, labda Shetani anakwambia wewe kuwa hauwezi kurudishwa tena. Yeye anadanganya, hakika, anafanya hivyo.) Kwa sababu, tazama, kama kuna wito wenye kilindi, ukiita, lazima kuwe na kilindi cha kuitikia wito huo. Kama kuna njaa kwa ajili ya Kitu fulani, hicho kitu chapaswa kiweko mahali fulani au hungekuwa na njaa kwa ajili yake. Ona?

102 Kama vile nimesema mara nyingi. Kabla samaki hajapata kuwa na pezi mgongoni mwake, ilipaswa kuwe na maji kwanza ya kuongelea au yeye hangekuwa na pezi yo yote. Kabla hakujakuwepo na mti wa kumea ardhini, ilipasa kuwepo ardhi kwanza kabla mti haujakuwepo, kwa sababu dunia ilipaswa kuwepo kwanza kusudi mti umee.

103 Sasa, kusijakuwepo kiumbe, ilipasa kuwepo Muumba akaumbe viumbe hivyo. Mwafahamu ninalokusudia? Sasa, mradi unataka na kuonea njaa kumrudia tena Mungu, kuna Mungu mahali fulani anayekuita, ona, au haungekuwa ukiona njaa. Muumba yuko!

104 Sasa, kama una . . . Kuna mahali ambapo unaweza kuvuka ambapo huwezi kurudi, lakini hapo ni kuwa chini pale tena katika hali ile ile uliyokuwamo. Inaonyesha kuwa *ulianguka* tu toka kwa neema. Kuanguka si *kupotea*. Nataka mtu ye yote

aniambie ambapo kuanguka ni *kupotea*, na aithibitishe kwa Biblia. Aliyeanguka hajapotea, yeye ako tu nje ya ushirika.

105 Israeli walianguka lakini hawakupoteza agano lao, walipoteza sifa za—zao pamoja na furaha.

106 Daudi alipoteza furaha ya wokovu wake alipomtwaa Bath-sheba, mke wa Uria, lakini yeye hakupoteza wokovu wake. Yeye hakusema kamwe "unirudishie wokovu wangu," kasema, "Unirudishie furaha ya wokovu."

107 Ee, kuna huu ushikiliaji sheria mwingi siku hizi, lile "usiguse, usionje." Haufanyi vitu kisheria.

108 Sikuja kanisani humu usiku huu kisheria. Najisikia mchovu, ni—ni—nimekuwa na wasiwasi, nimehangaika, sijui yaliyo hapa mbele yangu, moyo wangu unanichoma, zaidi sana hata moyo wangu una—unadundadunda. Nina kiharusi, uchungu, dakika ii hii, unanichomachoma huku na huko, juu chini kupitia *hapa*. Mdhaifu, mwenye mashaka, natetemeka; inashika *hapa* na kuminya; vidole vyangu vimebanwa na viatu vyangu. Sikujisikia kuja huku kamwe. Sababu gani nilikuja, basi? Kwa sababu nampenda Mungu. Niishi nife, yanipasa nisimame hapa kwa ajili Yake. Si kwa sababu ni lazima. Yeye hangejali kama nalitenda hayo au la. Ninge-. . .Kama ningelikufa ningeenda Mbinguni, haidhuru. Lakini ninakuja kwa sababu ninampenda. Mnamtumikia Mungu kwa sababu mnampenda, si kwa sababu yawapasa kufanya hivyo. Kwa sababu mnampenda kutosha!

109 Mimi si mwaminifu kwa mke wangu kwa sababu nasikitika yeye atanitaliki. Mimi ni mwaminifu kwake kwa sababu nampenda. Hakuna mwanamke mwingine ulimwenguni ila yeye. Hiyo ndiyo sababu mimi ni mwanaminifu kwake. Si kwa sababu . . .Kama nimefanya kosa nao walidhani nimefanya kosa fulani, nimjie, niseme, "Meda, mpenzi, sikukusudia kufanya hivyo." Yeye angenisamehe hayo, najua angefanya hivyo. Ningemsamehe; nampenda. Bali mimi—mimi ningemsamehe; yeye angenisamehe. Lakini singalitenda hayo kwa vyo vyote vile, nampenda sana kutenda hayo. Si kwa sababu sikudhani yeye angenisamehe, ni wazo kwamba nampenda sana hata singaliweza kufanya hilo. Mradi tu ninampenda hivyo, sitafanya hivyo kamwe; na kama yeye ananipenda vile impasavyo, yeye hatafanya hivyo pia.

110 Na unapompenda Bwana kwa moyo wako wote, haikupasi uwe na wasiwasi kuhusu mambo haya. Ukifanya kosa, hautendi dhambi kusudi, ndiyo kwanza umefanya makosa. Ona, umeteleza. Kweli ulikuwa juu hapa katika ushirika, umeanguka chini katika mchafuko huu chini hapa tena.

111 Lakini ni nini? Ni kama tu tai. Wakati mmoja niliona . . . juu hapa kwenye hifadhi ya wanyama ya Cincinnati, nilienda na Sara na nilikuwa naenda pale. Kama mna jambo nilipata kuona lililonidhuru, ni kuona kitu kilichofungiwa zizini.

112 Siwezi kustahimili kuona cho chote kwenye kizimba, hata ndege wadogo. Nami najua ninyi wanawake mna hao ndege wadogo, waachilieni waende.

113 Nilipokuwa mvulana mdogo nilizoea kusema, "Nikipata nafasi, nitakapokuwa mtu mzima, nitajipenyeza katika kila nyumba na kuachilia maskani hao wanyama wadogo." Naam, bwana. Nilisema... Nikiketi juu pale kwenye jua kali, nao wakisema, "Haa, haa, haa," huku huyo mwanamke amejilaza kule ukumbini anavuta sigara, na maskini ndege huyo mdogo ameketi pale akichomeka. Yeye hawezi kujisaidia, hana budi kuketi pale. Naye hakuzaliwa kwa ajili ya hayo! Niliwazia, "Wee, kama ningeingia juu pale nikamfungulie, yeye hangekuwa pale kwa muda mrefu." Ona?

114 Nachukia kuona kitu cho chote kimefungiwa zizini. Nachukia kumwona mtu anayejiita Mkristo na huku yumo zizini mwa kanuni za kanisa fulani, "Siwezi kusema, 'Amina'. Si—siwezi kuamini *Hayo*. Mchungaji asema, 'Usiamini Hilo." Lo, jamani! Ulizaliwa huru.

115 Ndipo na tai mkubwa je? Yeye ni ndege wa kimbinguni. Yeye huishi juu sana ya mawinguni. Huko ndiko aendako asubuhi. Juu sana, hakuna cho chote kinachoweza kumfuata! Hamna ndege mwingine... yeye angevunjikia angani vipande-vipande kama angejaribu kumfuata. Yeye ni ndege aliyetengenezwa kimaalum.

116 Kisha mtu fulani alikuwa amemnasa katika mtengo uliotengenezwa na mwanadamu, alikuwa amemnasa huyu tai mkubwa na kumweka katika hiki kizimba. Na maskini ndege huyu... Nilimtazama na moyo wangu ulinichoma tu. Yeye alitazama upande *hivyo* asijue jinsi ya kutoka humo kizimbani. Alikuwa tu... akaenda upande mwingine pale, naye—yeye alijua jinsi yeye angeruka, naye angeanza kutapatapa mabawa yake. Na hapa yeye angeruka, alikuwa akigongesha kichwa chake juu ya mtaimbo na kuvua manyoya toka kwa mabawa yake, manyoya ya mabawa, kote kichwani, hata kilikuwa kikitokwa na damu. Yeye aligonga mtaimbo huo kwa nguvu sana hata ungemtupa chini na kumlaza kichalichali. Naye angelala pale na afingirishe hayo macho yenye uchovu, atazame juu kuelekea angani, "Huko ndiko kwetu. Huko ndiko nyumbani kwangu. Huko ndiko nilikozaliwa. Lakini, tazama, kati yangu na kule mna kizimba. Vema, kitu pekee ninachojua, nimeweka nia yangu kwako na mimi hapa naja," na "puu," angelazwa kichalichali tena.

117 Niliwazia, "Jamani, si hilo ni baya mno! Laiti wangaliniuzia huyo. Ningetia rehani motokaa yangu ya Ford kumnunua, ona, kusudi nimwachilie." Ona? Lo, ilinifanya nijisikie vibaya sana, huyo maskani ndege mkubwa pale, manyoya yamemtoka... Niliwaza, "Hilo ndilo baya mno nililowahi kuona."

118 La, samahani, kitu kiovu mno nilichowahi kuona ni mtu aliyezaliwa kuwa mwana wa Mungu halafu amefungiwa zizini mwa kanuni fulani za imani. Naye anatazama juu pale na anamwona Mungu ambaye yeye hakika anataka sana kumtumikia, lakini yeye hawezi kufanya hivyo. Hawawezi kumruhusu kufanya hivyo, amefungiwa zizini. Hilo ni jambo la kuogofya mno.

119 Naam, ndivyo dada, ndugu, ye yote yule aliyeandika hili, kama umeanguka chini *hapa* hilo halimaanisha umepotea. Wewe ni tai tu aliyeingizwa tunduni, hivyo tu. Umefungiwa zizini chini hapa katika dhambi tena. Hutaki kuwa pale, hiyo ndiyo sababu unatazama juu. Naam, "Ewe Ndugu Branham, wakati mmoja niliishi juu pale, je, kuna njia hapa?" Naam.

120 Yanikumbusha mimi siku moja (ee, mvulana mdogo) nilikuwa nikitembea-tembea upande wa nyuma wa shamba, na kulikuwa. . .mtu fulani alikuwa amemfunga maskini kunguru mmoja amzuie asile mahindi. Na maskini kunguru huyo nusura afe kwa njaa. Singekuwa mchoyo hivyo kufanya hivyo. Yeye alimfunga maskini kunguru huyo mguu, na ndege huyo alikula kila kitu kilichokuwa mahali pale, hangepata kitu kingine. Mkulima yule alimwacha tu. Naye alikuwa mnyonge sana hata ha—hangesimama. Yeye tu. . .Nao hao kunguru wangepuruka juu na kusema, "Kou, kou, kou." Yaani, wanasema, "Kuja, kunguru Yohana! Majira ya baridi yanakuja, hima twende zetu kusini!" Lakini yeye hangefanya hivyo, alikuwa amefungwa.

121 Kwa hivyo siku moja mtu mmoja alipitia hapo na akamwona maskini kunguru huyo, kwa hivyo akaenda kule akamshika akamfungua, kasema, "Nenda zako basi, uko huru." Ona? Na kwa hivyo basi, muda si muda, yeye aliendelea kuzunguka pale.

122 Hapa kukaja kunguru, wakipaza sauti, "Njoo, kunguru Yohana! Kou, kou, kou! Twende zetu kusini, majira ya baridi yanakuja. Utagandamana kwa baridi hata ufe."

123 Kama yeye angetazama nyuma, asema, "Siwezi." Ona, yeye alikuwa amezoea kufungwa sana, ona, yeye alidhani tu alikuwa bado amefungwa.

124 Huenda ukadhani umefungwa, pia, ndugu, dada, uliyeandika swali hili. Huenda ukadhani Shetani amekufunga chini pale, lakini yeye anadanganya. Hapo kale Mtu mmoja alikuja duniani, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Yeye akakufungua. Basi, usiamini hayo, haikupasi kukaa chini pale, la, bwana, uko huru. Naam. Yeye alikufa mahali pako kuondoa dhambi zako. Basi mwamini tu yeye tu, tapatapa mabawa yako ukaruke pamoja na wengine wote. Usikae humo shimoni mwa Shetani. La, bwana.

Sasa, utaweka mikono yako juu yangu na niwe huru kwa hayo?

125 Dada mpendwa au ndugu mpendwa, hakika, ningeweka mikono yangu juu yako, lakini hilo halingekuweka huru. Kile kingekuweka huru, una. . .ni kufahamu kuwa wewe hakika umeshakuwa huru. Wewe umekwisha funguliwa. Haikupasi kuhangaika kuhusu kuwa huru, wewe umeshakuwa huru! Yesu alikuweka huru. Usifungwe tena na nira ya utumwa. Wewe u huru uwezavyo kuwa. Haikupasi kufungamanishwa. Kuweka mikono yangu juu yako ni desturi tu. Huenda tukafanya hivyo. Hayo, naam, ningefanya hivyo, lakini hilo bado halingekuweko huru hata ukubali yale Yeye amekufanyia; hayo ni mimi tu nikisema, "Bwana, naamini."

126 Vema, weka tu mikono yako kwa imani juu Yake useme, "Bwana, naamini," utainuka juu. Naam, ungama dhambi zako. Ona, "Afichaye dhambi zake hatafanikiwa, afunikaye dhambi zake, bali yeye aziungamaye dhambi zake. . . " Hapo ndipo unapopata uhuru na kuhesabiwa haki, unapokuwa tayari kusema, "Nimetenda dhambi, nimekosea." Hayo ndiyo uliyosema hapa:

> **Nimeanguka, nimetenda dhambi. Nimekosea kabisa! Kuna uwezekano kwangu kurudishwa upya tena?**

127 Kabisa! Mara unapotaka Hayo, hiyo yaonyesha kuwa Mungu amekutupia Kamba ya Kuokolea kukuinua wewe juu. Basi inuka tu kwa Kamba Yake ya Kuokolea ya imani na maombi, songa mbele hata uingie waliko tai wengine hivyo, wakiruka. Naam.

128 Naam, kuwekewa mikono, hilo—hilo ni jambo kuu, naamini hivyo. Naamini katika kuwekewa mikono, hakika naamini. Lakini hilo silo linalotenda hayo. Ningeweka mikono juu ya watu, juma baada ya juma, na bado halingefaidi hadi ukubali yale *Kristo* alikufanyia. Huko ni kukubaliana kwangu tu, kuwekea mikono. Waliwawekea mikono wazee. Walifanya mambo hayo, ilikuwa kibali chao mbele za Mungu kwamba wanatoa imani yao kwa hayo, wanatoa imani yao kwa hayo. Ona? Wakati mwingine, vitu kama . . .

129 Mimi hukosa kufahamika sana mara nyingi sana. Nina—nina. . .usiku uliopita. Nimekubwa na mashaka, na si—sijui nigeukie wapi. Ni—mimi, mwenyewe, nina mashaka, si—sijui la kufanya. Natumai hili ni kanisa tu la kawaida, au kanisa la kiroho linaloketi hapa, samahani, sidhani wanananasa haya kwa hivyo nitasema tu yale ninayotaka. Wao . . .

130 Nilitaka maongeo ya moyo kwa moyo pamoja nanyi, nami naamini nitayachukua tu, haidhuru. Nilikuwa na kijikaratasi hapa kilichokuwa kimeandikwa Maandiko, kama. . .Kama sikuwahi, ilikuwa niongee kuhusu *Ule Uinjilisti wa wakati wa Mwisho,* Uinjilisti wa wakati wa mwisho ni nini. Labda nitauweka huo kwa ajili ya siku nyingine. Ningependa kuongea nanyi toka moyoni mwangu, toka tu kilindi cha moyo wangu.

131 Nina mashaka, sijui nigeukie wapi. Nataka maombi yenu. Hii rairai ndogo hapa, juu ya haya—juu ya mambo haya, ilikuwa tu kusudi nipate nafasi ya kuongea nanyi dakika chache. Jambo lingine ninalotaka kuwaambieni, ona. Najua ya kwamba tuko karibu sana kwa jambo fulani. Sasa, msifahamu kwa kosa, msifanye hivyo. Ona?

132 Mtu fulani alikuja kwangu majuzi na kunifanya nijisikie vibaya sana. (Niliwaza, "Hakika sijakuwa mlegevu hivyo katika mafundisho." Ona?) Yeye alisema, "Ndugu Branham, katika muda wa siku kadhaa itanibidi kupasuliwa, siku kumi na tano zijazo, siku ishirini." Kasema, "Je, wadhani Yesu atakuwa amerudi, isinibidi hata kufanyiwa upasuaji?" Ona? Mwaona, unaifahamu vibaya. Usifanye hivyo! Ona, usifanye hivyo. Yesu huenda asije kwa miaka mingine elfu tano. Sijui. Hata hivyo huenda akawa hapa usiku huu. Huenda akaja kesho. Sijui atakuja lini, hakuna mwingine ye yote ajuaye. Hakika, hata Yeye Mwenyewe hajui. Hivyo ndivyo alivyosema. Hakuna mtu ajuaye.

133 Lakini mlijua Paulo alimtarajia Yeye kuja kila siku? Yohana, kwenye kile kisiwa cha Patmo, alidhani yeye angeishi kuiona. Ireneo alidhani hakika Yeye angekuja katika siku zake. Na wengineo wote, Polikapu, mtakatifu Martin, na wote katika nyakati zote. Luther aliwazia, "Hakika ndio huu!" Wesley alisema, "Huu ndio wakati ule." Charles Finney, John Knox, Kalvin, Spurgeon, kila mmoja wao alisema, "Huu ndio wakati ule!" Billy Sunday, na kuendelea hata wakati huu hapa, kila mmoja, "Huu ndio wakati ule!"

134 Tunautazamia. Hatujui wakati huo utafika lini. Ninaamini wakati ule ndio huu, nami nataka kushikilia mwenge, Nuru iangaze. Basi sikizeni, nina . . . Shikeni hili sawasawa! Nataka kuishi kila wakati wa maisha yangu kana kwamba namtarajia Yeye wakati uo huo, lakini nataka kuendelea kama kwamba ingalikuwa miaka elfu kumi tangu sasa. Ningali bado nataka kupanda mbegu, kuvuna mavuno. Nataka kuhubiri Injili na kuendelea tu kama nilivyofanya kila mara. Vivyo hivyo, huku macho yangu yameinuliwa yakikesha; yakivuta susu za . . . yakikusanya mavuno, ile nafaka. Ndiposa mwaka unaofuata nitavuna mavuno yangu tena, "Bwana, nilidhani ungekuja mwaka uliopita, lakini kama hukuja, huenda ukaja mwaka huu. Kwa hivyo nitapanda mimea yangu nipate kuwalea watoto wangu. Ukikawia, watapata chakula, usipokawia, nitakuwa nikikutarajia." Naam, ona, endelea tu kama kawaida.

135 Kama nilidhani Yeye angekuja asubuhi, usiku huu ningehubiri ujumbe ule ule ninaohubiri sasa. Kama nilidhani Yeye yuaja asubuhi hii, singelienda nikauze gari langu, singeenda kufanya *hili, hilo* au *lingine*. Ningeendelea tu kama kawaida, kwa sababu kila wakati ninamtazamia Yeye kuja. Kwa sababu Yeye huenda akaja tu kwa ajili yako, huenda ikawa usiku

huu ndio wakati wako. Labda usiku huu ndio wakati wangu. Sijui. Lakini moja yayo itakuwa saa yetu.

136 Na kuna tofauti gani kama ninaishi hapa au nimezikwa kule? Maana kama nimekwisha lipa adhabu ya mauti, nitakuwa kule kabla ya mtu ye yote aliye hai. Hiyo ni kweli. "Nasema haya," 2 Wathesalonike sura ya 5, "Nawaambieni haya kwa maagizo ya Bwana. Kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata kuja kwa Bwana hatutawatangulia au kuwazuia wao waliokwisha kulala mauti. Maana parapanda ya Bwana italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza," majaliwa ya wale waliolala mauti watafufuka kwanza. Hivyo ndivyo tujuavyo kuwa kumekaribia, ona. "Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, na tutanyakuliwa pamoja nao, ili tumlaki Bwana hewani."

137 Kwa hivyo kuna tofauti gani kama ningalikufa katika ule wakati wa Nuhu, kama ningalikufa katika wakati wa Ibrahimu, kama ningalikufa katika wakati wa mitume, kama ningalikufa majuma mawili yaliyopita au sasa hivi? Ina tofauti gani? Nitakuwa kule katika dakika moja, kufumba na kufumbua, ninapumzika tu hata wakati huo.

138 Sasa, kukusanyika kule kutakuwa kwa Bwana, kama Yakobo, katika sura ya 49, yeye alisema, "Yeye, Mwenye Milki atakapokuja, na kukusanyika kutakuwa Kwake. Hakutakuwa na mfanya sheria hata. . .toka kati ya miguu yake, hata atakapokuja Yeye Mwenye Milki," akinena habari za Yuda, "ambaye watamkusanyikia."

139 Sasa, watu wengi sana wanatazamia kanisa fulani, kundi kuu la watu watakaonyakuliwa pamoja, kanisa fulani, dhehebu fulani, kanuni fulani ya imani kunyakuliwa. Sivyo. Sivyo ilivyo kwa vyo vyote vile.

140 Kule kukusanyika kwa watu, Mungu atakapoliita kundi Lake pamoja, huenda akachukua wawili toka Jeffersonville, wawili toka Indiana, wawili toka Kentucky, wawili toka Mississippi. Hivyo ndivyo alivyosema hasa; si kwa maneno hayo, ila Yeye alisema, "Wawili watakuwa shambani," hiyo ni mchana, "nitamtwaa mmoja na kumwacha mmoja. Wawili watakuwa katika kitanda kimoja," upande mwingine wa dunia ni usiku, "Nitamtwaa mmoja nimwache mwingine." Ona?

141 Kukusanyika kule kwa watu hakutakuwa kwa kikabila, kundi fulani hapa. Itakuwa ufufuo wa kukusanyika kote duniani, na kunyakuliwa kutakuwa vivyo hivyo. Kwa sababu Yeye alisema, "Mmoja alipolala katika zamu *hii* mwingine katika zamu *ile,* mwingine katika. . .na kuendelea hata kwa ile zamu ya saba. Ndiposa atakapokuja Bwana arusi hao wote wataamka, kila mmoja, wote toka Mwanzo hata mwisho wa Ufufuo. Kila mmoja wao akaamka, naam, kujitayarisha kuingia."

142 Sasa, waona, Yeye aonyesha kuwa wote waliokufa watafufuka toka makaburini, katika kuja Kwake, yule mwenye haki, yule Bibi-arusi, wale waliolala kaburini watafufuka kwenye ufufuo ule. Kisha anaonyesha kuwa watu wanaoishi duniani, itakuwa mmoja *hapa* na mmoja *pale,* haitakuwa kundi la watu waliokusanyika pamoja katika kundi ndogo. "Kwa kuwa mmoja atakuwa shambani, au wawili shambani, nitamtwaa mmoja nimwache mwingine," pale laja mojawapo wa kanisa wakati wa mchana. Sehemu nyingine ya dunia, "Wawili watakuwa kitandani, nitamchukua mmoja nimwache mwingine." Sivyo?

143 Kwa hivyo kukusanyika kule kutakuwa Kwake Kristo au niko Jeffersonville, au niko Sweden au niko . . . Po pote pale, kukusanyika kutakuwa kwa Mchungaji yule. Ona? Ndiposa tutanyakuliwa sote pamoja na waliofufuka kumlaki Bwana hewani. Watu watakuwa wakija toka sehemu zote za dunia, hao ni walio hai. Watu waliokufa, na kadhalika, watafufuka. Kisha Kanisa lile litanyakuliwa (pamoja) kumlaki Bwana hewani. Ona?

144 Kuja Kwake kutakuwa kwa dunia nzima. Haitakuwa tu kuja Louisville. Haitakuwa tu kuja kwa Wabatisti, kwa Wapresbeteria. Itakuwa "Wenye moyo safi watamwona Mungu," na kufufuka kule na kukusanyika kule kutakuwa toka kila mahali.

145 Basi, sasa, itakuwa lini? Labda usiku huu, labda kesho, labda mwaka huu, labda miaka hamsini, labda miaka mia, labda miaka mingine elfu. Sijui. Hakuna ye yote ajuaye. Lakini hebu—sisi, mimi na wewe, tuishi usiku huu kama kwamba itakuwa usiku huu.

146 Lakini, sasa, katika kutenda kama mlivyosema, "Ni—nitafanyiwa upasuaji." Vema, kama huna budi kupasuliwa, huna imani ya ukombozi, nenda zako kafanyiwe upasuaji wako.

147 Kama nilikuwa naenda kununua ki—ki . . . Mtu fulani alikuja na akaniandika kijikaratasi hivi majuzi, akasema, barua m—mrefu, akasema, "Ndugu Branham, sijui la kufanya." Kasema, "Mimi na mke wangu tumekuwa waaminifu sana kwa Mungu tuwezavyo kuwa. Tumewalea watoto wetu." Kisha kasema, "Sasa, inayonitatiza," kasema, "tuna . . . tumelihifadhi shamba, tumenunua shamba." Lakini kasema, "Jinsi tunavyolipenda: kuna kijito kinachopitia mahali pale." Ilikuwa kule Oregon. Halafu kasema, "Tunasikia kuwa unakuja Oregon. Nitakwambia kile tumeamua kufanya. Tunajua kuwa . . . Tulidhani tungelinunua kwa ajili ya watoto wetu, kwa sababu hakuna ye yote wao aliye Mkristo." Kasema, "Tulidhani tungewanunulia kwa sababu itawapasa kuwa humu katika wakati wa ile dhiki iliyo kuu, na kuwanunulia kuwaacha wakiwa na kitu fulani, kwa maana tunaamini tutakuwa katika

Kunyakuliwa kule. Kwa hivyo hatujui la kufanya kuhusu hilo, kwa hivyo labda ukija labda tutakupa wewe shamba hilo, ona, ndiposa utalifanyia cho chote utakacho."

148 Nilijibu, nikasema, "Ni vizuri jinsi gani kwenu kuwaza juu ya watoto wenu."

149 Kasema, "Mimi na mama huenda nje kule, wakati wa jioni." Kasema, "Niko tayari kustaafu, na" kasema, "jinsi tulivyo na wakati wa kustarehe, kupitia shambani, kutazama ile chemchemi, na kusimama nje pale tukimsifu Mungu."

150 Nikasema, "Endeleeni kufanya hayo, ishi tu hivyo, kimwili, kifedha. Endeleeni tu kujitahidi hata atakapofika. Ona, endeleeni tu kukaa hapa, endeleeni tu hata atakapofika."

151 Panga, endelea, fanya hayo, "Bwana akipenda! Bwana akipenda! Nitafanya *hili* Bwana akipenda." Huenda akaja kabla ya wakati huo. [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] Lakini endeleeni jinsi mnavyoendelea hata . . . Lakini itengeneze nafsi yako, kwa kuwa, Yeye aweza kuja dakika yo yote. Ona, iweni tayari. Kwa kuwa, mwaona, Yeye huenda akaja kwa ajili *yako* dakika yo yote, sekunde yo yote, mdundo unaofuata wa moyo, kupumua kunakofuata, Yeye aweza kuja kwa ajili yako. Lakini endelea tu kufanya cho chote unachotaka kufanya, mradi tu ni cha kweli na kiadilifu na kinyofu, endelea kukifanya.

152 Sasa, twajua kuwa tunakabiliana na kitu fulani. Najua hivyo: mwajua hivyo. Si—si—sijui nielekee upande upi, mwakumbuka yapata miaka minne iliyopita, katika Chicago siku moja, Roho wa Bwana alinijia kasema, "Imekwisha! Na ufufuo umekwisha, na Amerika imetupilia mbali nafasi yake." Yako kwenye kanda. "Na haitakuwako tena. Imekataa nafasi yake ya mwisho."

153 Nawatakeni mchunguze. Je, ye yote wenu ajua siku gani hayo yalinaswa kwenye ukanda? Tunayo. Leo na Gene wanayo. Niliisikiza hapa muda mchache uliopita. Boze aliyaandika katika gazeti lake. Na kwa hivyo tazameni yaliyotendeka tangu wakati huo, ona, ufufuo umekoma.

154 Nilisema hayo kule kule Blue Lake usiku uliopita, kisha maskini mtu mmoja akarudi asubuhi iliyofuata, kasema, "Ndugu Branham huenda akasema Wapentekoste wamekoma, lakini si mimi! Mungu atukuzwe! Haleluya," na kuendelea na kuendelea. Ona, lakini maskini mtu yule hakujua alikuwa anapiga pembe upande upi. Ona, yeye hafahamu. Ona, yeye hajui. Ni sawa, kuwa mwenye shauku, hiyo ni sawa hasa.

155 Lakini tazama kila mahali! Wanafanyaje? Imekuwaje kwa hawa watu? Imekuwaje kwa ufufuo? Imekuwaje kwa Billy Granham, Oral Roberts, wengineo? Ufufuo unaendelea wapi? Umekwisha! Moshi umetulia. Mbegu zimepandwa. Mkutano umekwisha. Mioto imepoa. (Katika hekalu la kale la Rumi, katika sherehe za Vesta, moto ulipozimika wafanyi biashara

walienda zao nyumbani, pale madhabahuni.) Sasa, twaona ufufuo haupo. Si kuwa na shauku.

156 Ndipo nawazia kuhusu mtoni kule katika mwaka wa 1936, nawaza yale Yeye alisema. Nini ilitendeka pale? Wengi wenu mwajua. Nilikuwa tu mvulana, na nikiwabatiza ubatizo wangu wa kwanza wakati malaika wa Bwana aliposhuka na kusimama pale nilipokuwa. Watu wengine walisema. "Hakumwona." Kisha sayansi ilithibitisha kuwa ilikuwa kweli. Ona? Ona?

157 Sasa, Yeye alisemaje kule? "Kama ilivyokuwa, kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utatangulia kule kuja kwa pili."

158 Nimeyatazama hayo kote duniani, yamezunguka kote duniani. Karibu tu mara moja, mikutano ya ufufuo ilianza kila mahali. Mioto ya ufufuo ilikuwa ikiwaka kila mahali, kumekuwa na ufufuo mkubwa sana tuliowahi kujua. Lakini kulikuwa na lo lote hapo mbeleni? Hata moja! Yapata majuma mawili hapo awali, nilimsikia mtu akitoa hotuba katika New Albany, kasema, "Watu walikuwa wakiamini zile fujo za—za ufufuo, kama Billy Sunday na wengineo." Kasema, "Tunajua hakuwezi kuwa na zaidi ya hayo, watu wanataka ushuhuda thabiti. Hakuna kitu kama hicho!" Walipokuwa wakifanya fujo hizo kuu, wakati ule ule Mungu akatuma mlipuko mkuu sana wa ufufuo tuliopata kuwa nao tangu zile karne za mwanzoni, watu wengi zaidi wamekwisha okoka (mamilioni).

159 Tarakimu yaonyesha kuwa ujumbe wa mtu ye yote hudumu kwa miaka mitatu, ye yote yule, kisha yeye huishi kwa sifa zake wakati uliobaki hata Mungu anapomwita. Naam, imekuwa hivyo tangu Kristo, Yake ilikuwa mitatu na nusu, ona. Na yaonekana vivyo hivyo kila mahali, Spurgeon, Knox, Calvin, na kadhalika, inaonekana kwamba miaka mitatu hadi mitatu na nusu ndio kikomo cha huduma ya mtu. Nyingine yote. . . Mshumaa wake umechomeka, yeye anaishi kwa sifa zake zilizopita, kama alikuwa mwovu, kazi zake—kazi kumfuata; kama yeye amekuwa sahihi, kazi zake zinamfuata. Hivyo tu.

160 Sasa, hilo lilimaanisha nini? Nimekuwa nikihubiria kanisa hili hapa na kuwaambia ninyi kwamba "Naamini kuna mtu mkuu anayekuja." Naamini na nimeshawaambia kwamba "Naamini kuwa Maandiko yanaunga mkono kuwa kutakuwa na mjumbe wa wakati wa mwisho wa kanisa." Naamini hayo. Nimemtazamia mtu huyo kuonekana, nimemtazamia daima.

161 Nami nimeona mtu akiinuka, namsikia, mtu mkuu anaanza kuvuma, naona ujumbe wake uko mbali sana na Biblia. Namwona akiruka tena pembeni. Ona? Namtazama mwingine akiinuka, anaruka kule juu, bali haingii kati ya tai, yeye anakaa kati ya kunguru wa kidhehebu. Anakaa chini *hapa* dhehebu lake, na mwingine anaongeza wafuasi zaidi na kadhalika. Naitazama, naona ikififia.

162 Nawazia, "Mungu, yuko wapi yule atakayeigeuza Imani ya baba iwaelekee watoto wao? Mbegu zile zitapandwa wapi? Ziko wapi? Itakuwaje?"

163 Sasa haya ndiyo matokeo yake. Kama—kama ujumbe huo pale mtoni siku hiyo, kama ndio huo, kule Kuja kwa Bwana kumekaribia, kuko karibu. Kama sivyo, huwa shwari kabla ya tufani. Sijui. Yeye hajanifunulia. Ninajaribu kushangaa, "Je, huo ndio uliokuwa Ujumbe Wake Halisi? Hayo tu ndiyo Yeye alitaka niseme? Hapo ndipo alipotoa agizo? Ni hayo tu? Kama ni hayo tu, tumekaribia sana, sana. Imechelewa kuliko mnavyowazia." Kama sivyo ilivyo, basi huwa shwari kabla ya dhoruba.

164 Sasa, mtu fulani aliniandikia mimi hapa si muda mrefu uliopita, akaniuliza, kasema, "Kama huamini kuwa kanisa litapitia katika wakati wa ile Dhiki iliyo kuu, na Ufunuo 13 je, jinsi walivyoshinda kwa Damu ya Mwana-Kondoo na ushuhuda wao?" Mtu huyo akauliza swali hilo. Nashangaa. Je, mwatambua kuwa sura tatu za kwanza za Ufunuo zinashughulika na Kanisa katika ule Wakati wa Kanisa? Huo ni wakati wa ile Dhiki, na si wakati wa Kanisa; kanisa litanyakuliwa na kutwaliwa juu katika sura ya 4 ya Ufunuo, halirudi tena hata sura ya 19 linapokuja pamoja na Yesu. Hiyo ni kweli Huo ni wakati wa ile Dhiki, haukusiani kamwe na lile Kanisa kwa vyo vyote vile.

165 Ahadi hizi zote kuu za mambo makuu ambayo mmeona katika Biblia kama yale yatakayotendeka, hayo ni kule katika ufalme wa Wayahudi, si hapa kati ya Mataifa. Naamini watakuwa na mkutano pamoja na huyu anayetazamiwa kuja na kurudisha Imani ya watu, ambayo imeahidiwa. Na njia pekee niwezayo kupata hilo, ni kwa sababu Yeye alisema, "Mara tu baada ya Ujumbe huu, ya kwamba, dunia itateketezwa kwa joto, moto." Hebu niwasomee hayo kwenu hali tukiwa papa hapa, na chunguzeni yale isemayo.

166 Na sasa huu ujumbe mdogo wa Ufalme, labda huenda nikahubiri huo Jumapili asubuhi, yakiwa mapenzi ya Bwana, ona, na Bwana akipenda.

167 Sasa tazama hapa, huku ni kule kuja kwa Yohana, Malaki 3:

> *Angalieni, na...mtuma mjumbe wangu, naye... namtuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu; naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafula; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema, BWANA wa majeshi.*

168 Mwaona hiyo Malaki 3? Mathayo sasa, tazama Mathayo sura ya 11, na sikiza haya, na kifungu cha 6. Hebu tusome sasa Mala-...Mathayo 11, Yesu akinena. Na sasa hebu tuanzie sura ya 11:

Ikawa Yesu alipokwisha kuwaagiza wanafunzi wake kumi na wawili, alitoka huko kwenda kufundisha na kuhubiri katika miji yao.

Naye Yohana aliposikia huko . . . gerezani matendo yake Kristo, alituma wanafunzi wake wawili

Kumwuliza, Wewe ndiye yule ajaye, au tumtazamie mwingine?

169 Mwaona hiyo huzuni ya nabii huyo? Yeye alijua kitu fulani kingetendeka, lakini yeye hakuwa na hakika kilikuwa wapi. Ona? Ona, yale tu yaliyokuwa yakitendeka, "Wewe ndiwe Yeye Yule?" alipokwisha kumtangaza.

Yesu . . . akajibu akamwambia, Nendeni

mkamweleze Yohana mnayoyasikia na kuyaona;

Vipofu wanapata kuona, . . . viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, . . . viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema.

Naye heri awaye yote asiyechukizwa nami.

Na hao walipokwenda zao, Yesu alianza kuwaambia makutano habari za Yohana, . . . (Sasa sikiza!) . . .

Mlitoka kwenda nyikani kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na upepo? La, huyo hakuwa Yohana, Yohana haridhiani.

. . . mlitoka kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo? (Yaani, ukosi umepinduliwa ndani nje, mwajua, na walioelemika na watu mashuhuri) *tazama, watu wavaao mavazi mororo wamo katika nyumba za wafalme.* (Wale wawabusuo watoto wachanga, na kuwaoza vijana, na kuwazika wafu, na mwajua, au kuzurura huku na huko katika . . . ? . . . ni watu kama hao, yeye hashiki upanga ukatao kuwili. Ona?)

. . . Sasa, mlitoka kwenda kuona nini? Mtu na mavazi, yake, na akitikishwa *na upepo?*

. . . Mtu aliyevaa mavazi mororo? Tazama, watu wavaao mavazi mororo wamo katika nyumba za wafalme.

Lakini kwa nini mlitoka? Ni kuona nabii? Naam, nawaambia, na aliye mkuu zaidi ya nabii.

170 Tazama! "Huyo ndiye . . ." Sikiza sasa, haya ni Maneno ya Yesu mwenyewe:

Huyo ndiye aliyeandikwa hayo, Tazama, mimi namtuma mjumbe wangu mbele ya Imani Yagu, naye . . . uso*, naye ataitengeneza njia yako mbele yako.*

171 Sasa tazama malaki 3:

Angalieni, nam...tuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu;...(Malaki 3, si Malaki 4)

172 Sasa tazama Malaki 4:

Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru: na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao maovu, watakuwa makapi;...na siku hiyo inayokuja itawateketeza, asema BWANA wa majeshi,...hata haitawaachia shina wala tawi (huo ni wakati wa ile Dhiki na maangamizi, ona, inayokuja).

Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, Jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; (kule kuja kwa Bwana)*; nanyi mtatoka nje...*nanyi *mtatoka nje, na kucheza cheza kama ndama wa mazizini.* (hivyo ni kama kuenda malishoni, kuondoka)

...mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema BWANA wa majeshi.

173 Kwa maneno mengine, wenye haki, katika kurudi pamoja na Kristo duniani, watakanyaga hayo majivu. Mwonapo watu hawa, wenye kiburi, wenye majivuno, wanaodharau, wanaingilia yasiyowahusu, na hali wakidai kuwa Wakristo, wao si kitu ila majivu. Hivyo tu. Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo. Ona? Tazameni sasa.

Ikumbukeni...torati ya Musa, mtumishi Wangu, niliyomwamuru huko...Horebu kwa ajili ya Israeli wote, naam, amri na hukumu.

Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya: kabla tu ya siku hiyo (kule kurudi kwa Bwana), Eliya atakuja kwanza.

174 Vema, kumbuka, ingali usoni. Sasa, haingekuwa kule kuja kwa Yohana. Yeye alikuwa Eliya, lakini yeye yuaja mara tano, sasa. J-e-s-u-s, i-m-a-n-i, n-e-e-m-a. Ona, *tano* ni nambari ya "neema." Eliya atakuja mara tano: wakati mmoja ni Eliya; kama Elisha; kama Yohana; mwishoni mwa Mataifa; na kule akiwa pamoja na Musa kwa Wayahudi. Nambari kamilifu, nabii mkamilifu, mjumbe mkamilifu, mkali, hadari, Ona? Tazama:

...nitawapelekea Eliya...kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya.

Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana.

175 Ona, si kule kuja kwa kwanza kwa kumjulisha; huyo alikuwa Yohana, kwa sababu dunia haikuteketezwa kama makapi, wenye haki hawakupata kamwe kukanyaga majivu ya watendao uovu.

Lakini kabla tu haya hayajatendeka, Elisha atakuja. Naye atafanyaje? Ataigeuza Imani ya watoto iwaelekee baba zao, ile imani asili ya Biblia.

176 Nionapo mtu akija, nadhani, "Huyo hapana budi ni yeye. Mtu anapoanza kupata sifa, mtazame, anayeendea makanisa." Yeye anafanyaje? Yuko maili elfu kutoka kwa Biblia. Yeye anafanyaje? Anazurura hapa na pale, hewa yamtoka na anafifia. Ona, "Mwenye mfano wa utauwa, lakini akikana Nguvu zake, akikana ile Imani." Haamini Biblia, akisema, akishikilia kanuni za iamni, madhehebu, akipata watoto wa kidhehebu. Haina budi kuanguka. Ndiye huyo pale akirudi tena.

177 Yuko wapi yule atakayepanda ile mbegu kwa ajili ya hilo Kanisa la wakati wa mwisho? Iko wapi ile mbegu iliyoiva, yule Eliya aliyeahidiwa? Na mara tu baada ya siku zake ndipo ile Dhiki iliyo kuu itaanza na kuteketeza dunia.

178 Ndiposa Kanisa na yule Bibi-arusi watakaporudi, yule Bibi-arusi pamoja na Kristo watakanyaga majivu yao, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, dunia itakapotakaswa kwa moto. Ndipo wao watatawala. Na makafiri ambao hawajawahi kusikia Injili watafufuliwa katika wakati huo, na wana wa Mungu watadhihirishwa. Kama yeye atatawala, hana budi kutawala juu ya kitu fulani, yeye ana ufalme. "Nao wakitawala pamoja na Kristo," naye Kristo akitawala kwa fimbo ya chuma, mataifa. Ndipo Injili . . . Ndipo wana wa Mungu waliodhihirishwa, wakiwa na mamlaka kama aliyokuwa nayo alipokuwa hapa, ona, kutazuka ule Utawala wa Miaka Elfu katika Utawala huo, ona, juu ya majivu.

179 Kwa hivyo nimetazamia kitu fulani. Je, kimetupita kwa unyenyekevu nasi tumekikosa? Je, kimepita na kanisa limeachwa katika dhambi zake? Kama ndivyo ilivyo, basi kumechelewa zaidi ya unavyodhani. Kama sivyo, basi yuaja mtu mmoja mwenye ujumbe unaoambatana kabisa na Biblia, na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Mbegu zitaingia magazetini, vitabu, hata kila Mzao wa Mungu aliyechaguliwa asili ameusikia. Hakuna ye yote wao atakuja isipokuwa Baba amewavuta; na kila mmoja ambaye baba amemvuta atausikia na atakuja. Hivyo ni kusema, ile mbegu iliyochaguliwa asili italisikia Neno.

180 Kisha hayo yatendekapo, itakuwa kukusanyika pamoja. Na Yesu ataonekana, ndipo litaondoka Kanisa toka duniani kote hivyo, kwa ufufuo, kuenda juu.

181 Je, itakuwa kama Yohana alivyokuja, wala wanafunzi wateule hata hawakujua? Wao walisema, "Basi kwa nini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?"

182 Yeye alisema, "Yeye amekwisha kuja na hamkumjua." Lakini kasema, "Walimtenda yale waliyosema wangemtendea. Ujumbe wake ulikuwa wa haraka sana, tazama, kwa Israeli wote, na ilitendeka tu mahali pamoja padogo . . . mahali padogo pa—

pawili, chini tu ya Yerusalemu na pale, hata kule . . .? . . . ambapo Yohana alienda kubatiza, na papo hapo mtoni alipokuwa akibatizia, mto hou ulikauka. Miezi sita tu na kule kutangulia kwote kwa Masihi kukaingia. Ona?

183 Je, tumekosa kuona kitu fulani? Kumechelewa zaidi ya tunavyodhani? Haya ni maongeo ya moyo kwa moyo sasa. Haya ni kwa usiku huu tu, ku . . . Naam, ni—ni kuongea kwetu tu hapa. Je, kumechelewa zaidi ya mnavyodhania? Itakuwa lini? Sijui. Huenda ikawa usiku huu. Huenda ikawa miaka mingine hamsini. Sijui itakuwa lini, nitaendelea tu kama ninavyofanya sasa. Vema, ni nini? Je, natazamia kitu fulani?

184 Niliota ndoto ya ajabu usiku uliopita, imenihangaisha siku nzima. Kwa kawaida sioti sana. Lakini niliota ndoto . . .

185 Ningeenda kila mahali, na ilikuwa kwamba ningetangaza ujumbe huo na ningeona mmoja hapa na mwingine pale wakiushika. Ningerudi moja kwa moja tena na kueneza ujumbe huo nao wangeinua mapua yao na kuondoka. Imekuwaje? Wameshatenda dhambi hata siku zao zote za neema zikawaishia? Je, wa mwisho ameshaingia? Je, imekwisha? Je, tunangojea tu maangamizi? Je, hivi vita vyote vidogo vinavyoendelea hivyo ni vya matayarisho?

186 Jambo fulani linakaribia kutendeka. Kabla halijatendeka. Kanisa litakuwa limeondoka. Jinsi sikubali kuwa kanisa litakuwa katika ile Dhiki! Je, wawezaje kufanya mfano kutoka kwa kitu kisicho kamili? Ona? Nuhu alikuwa safinani kabla hata tone moja la mvua kunyesha. Lutu aliondoka Sodoma kabla moto ule haujashuka. Ona? Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku hizo ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Adamu atakapokuja." Kanisa halipaswi kusimama hukumuni, tayari liko katika Kristo.

187 Kile tunachohitaji ni kukamilishwa kwa watakatifu. Watakatifu hawafahamu, ona, wanakuwa . . . Hawajui la kuwazia, ona. Sasa tuna . . .

188 Kama hilo ni sahihi . . . Kama sivyo, jambo fulani litatendeka upesi, kutakuwa na mlipuko. Ninatazamia, sijui nielekee upande upi.

189 Usiku uliopita niliota ndoto. (Ndipo nitamalizia) Niliota ndoto, kitu kigeni mno . . .

190 Nilikuwa nimelala pale nikiongea na mke wangu, kuhusu kule kuja . . . Tulikuwa tumemaliza kuomba, nami . . . Mtu fulani, mzee Dallas, alikuwa amepiga simu ati alikuwa ameweka kitu fulani sikioni mwake, na nikaenda mle . . . Linatokwa na damu, naye ilimpasa aende upesi kwa daktari. Nami niliingia mle kuomba, na Roho Mtakatifu kasema, "Sawa" Ona?

191 Huyu hapa akija, ni vema. Daktari alisema, "Naam, nilidhani ulikuwa unaenda kupata . . ." Kasema, "Umeumiza

kiwambo cha sikio, kimepasuka, na damu inatiririka toka kwake, na kadhalika." Yote . . . Tuli—tuliporudi, yeye hakusema kitu. Hajui ni nini, ona, hakuna maambukizo, wala cho chote. Ona?

192 Kwa hivyo mtu fulani alikuwa amepiga simu, nami ningeingia chumbani mle na kuomba. Siku nyingine tena wangepiga simu, kasema, "Imekwisha. Barabara kabisa! Endelea!"

193 Nami nilikuwa nikiongea na mke wangu, nikasema, "Mpenzi, kwa karibu mwaka mmoja na miezi minne imekuwa vigumu kujua niende wapi." Nikasema, "Sijui nini." Yeye akasema . . . Tulikuwa tukiongea kuhusu kazi. Nikasema, "Sijui la kufanya, ninasimama nikishangaa. Je, tunatazamia . . . Je, huyo nabii mkuu wa Mungu . . . Anakuja jukwaani kulipua kitu kile? Je, yeye atajulikana kwa umma?"

194 Niliwaza, "Hilo ni kinyume cha Maandiko, kwa kuwa, 'yeye yuaja katika saa msiyoitarajia.'" Ona? Nami sijui la kufanya. Je, tumeshaipa kisogo? Nilidhani, "Sitaki kukaa hapa karibu na nyumba." Niliwaza . . . Nami natumai haya hayanaswi; kama yananaswa, ikate kanda hii itupilie mbali. Ona? Sasa yeye alisema, kama . . . Nilisema "Kama ndivyo ilivyo, sisi tuko karibu zaidi ya tunavyodhania."

195 Kuna kitu kimoja kilicho na . . . kitakachotendeka. Au kitu fulani kitatendeka kwangu sasa. Nami sioni sababu gani yeye hakuniruhusu niende nilipokuwa chini kule kwenye kiti kile hivi majuzi, ndipo, ona, kama hakuna lingine lo lote la kufanywa. Mbona? Mbona sikuenda? Ilikuwaje? Je, kuna jambo lingine la kufanywa? Niliwazia, "Vema, kama ni ujumbe wangu, watu watauinulia mapua."

196 Ndipo kitu fulani kinaniita mimi katika nchi za ng'ambo. Nasikia wito wa kwenda ng'ambo, ukitoka kila mahali.

197 Barua ilikuja tu hivi majuzi, Ndugu Ligger akiandika ki—kitabu juu ya mkutano wa Durban. Yeye alisema, "Hapajakuwepo na kama huo. Afrika haikuwa imeshawahi kuwa na mtikisiko kama huo. Katika usiku mmoja bara hili lenye giza la Afrika lilipata mtikisiko ambao hawajawahi kuwa nao maishani mwao." Hiyo ni kweli, kule kwa wale makafiri.

198 Nalitazama humu chini, nikaona hawa maskini watu weusi, watu wapendwa, nikaona jinsi watu hao walikuwa wakiwatendea wao kama . . . vibaya zaidi ya watumwa. Nilimwona maskini mvulana mmoja pale ambaye . . . nami . . . alifanya kazi kule, nami nilisema . . . Mvulana yule, hu . . . Ninyi wanawake hamngefanya kazi nyingi hivyo katika siku mbili au tatu, hata mkijitahidi vipi, kama kijana huyo ilivyompasa kufanya kwa siku moja. Yeye angelala kwa godoro lililojazwa majani makavu karibu na chumba kidogo kikuukuu cha kuogea (yapata urefu wa futi nne na upana wa futi nne), amejikunyata

mle. Naye alipata shilingi ishirini kwa mwezi, hizo ni dolla mbili na senti themanini. Naye hata hakula makombo toka mezani, ndoo ya unga wa mahindi; theluthi yake, kiamsha kinywa; theluthi yake kwa chakula cha kutwa; na theluthi nyingine usiku huo kwa chakula cha jioni. Alifanya kazi hata saa kumi au saa kumi na moja, thenashara; anaamka asubuhi inayofuata amshughulikie mtoto mchanga na kadhalika, na kupangusa vipandio na apanguze motokaa ya bosi wake. Na yule mama mkubwa, mzee aliyenona, hafanyi cho chote ila kuketi pale na kuyapamba makucha yake na kunywa chai, goigoi, hafai kitu.

199 Maskini kijana huyo ilimpasa afanye kazi nyingi sana. Yeye alipatwa na homa ya kukohoa, ilionekana kama alikuwa anasikia kukohoa, kama “Hau, hau, hau.” Na siku moja nilitazama pale, nikasema, “Je, si mumpeleke mvulana yule . . . Mbona hamumleti mkutanoni?”

200 “Yeye ni Kafiri” [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] Hilo maana yake ni “mlaghai.” Si ajabu wao huudhishwa na jina hilo sana. Ningefanya hivyo, pia. Mtu huyo ni ndugu yangu. Na ndiye huyo pale. Yeye si mtumwa. Rangi yake si kitu. Yeye ni ndugu yangu. Na ndiye yule pale hivyo.

201 Nikaondoka, nilimwita “Thomas.” Kijana yule angeongea lugha tatu. Nami nilisema, “Thomas?”

202 Yeye aligeuka, akaanguka magotini mwake na kuinua mikono yake juu, kasema, “Naam, bwana.”

203 Nikasema, “Amka. Mimi si bwana wako, mimi ni ndugu yako.” Nikamkumbatia kwa mikono yangu. Yeye akinitazama hivyo, na machozi makubwa yakitiririka mashavuni mwake. Nilisema, “Thomas.”

204 Na Roho Mtakatifu akaja kisha likatokea ono. Nilimwambia jambo fulani. Naye akasema, “Naam, bwana. Hilo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyokuwa.”

205 Nikasema, “Thomas, kukohoa kule kumekuondokea, hautakuwa nako tena.” Naye akapona.

206 Watu wakitia pesa mfukoni mwangu, nilikuwa na pauni mia na themanini ya sarafu zile (ni sawa na dolla mbili na senti themanini) Nami niliogopa kumpa; niliogopa bosi wake angempata nazo, wangedhani yeye aliiba kisha wangempiga hata afe. Ndipo ni—nikamwambia yule bosi, nikasema, “Ni—ninampenda mvulana huyo. Hebu nimpe pesa kidogo.”

“Ee, la! La! Utamharibu.”

207 Nikasema, “Wewe umeharibika kabisa.” Ona, “Mnafanya nini hapa? Hamfanyi cho chote. Mvulana huyo anafanya kazi yote na nusura mumuue kwa njaa. Yeye ana ma—mama mjane na dada mgonjwa, kisha mnampa dolla moja . . . dolla mbili na senti themanini kwa mwezi.” Nilisema, “Siku moja mtajutia hayo!

Kunao watu weupe milioni mbili na karibu watu weusi milioni mia. Mtakuwa na maasi."

Kasema, "Usiseme hayo nchini Amerika, yale yanayotendeka hapa."

208 Nikasema "Nani atakayeniambia ninyamaze? Mungu pekee." Kasema, "Si ajabu watu wale wana kinyongo, kwa kufanyiwa hivyo." [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] Naam. Nami niliwatetea.

209 Siku moja wahudumu kadhaa, ukosi uliopindiliwa, masharubu madogo, walikuja Rhodesia.

210 Maskini rubani mmoja aliyevalia kijani kibichi alinirusha katika moja ya tufani za tropiki, ndipo akaendesha maili mbili kama—kama . . . juu hewani, ikirukaruka. Hatukujua kama tulikuwa tumeketi juu chini; ile eropleni ikizunguka tena na tena na tena. Na hatimaye ili- . . . Hatukujua kama ilikuwa ikielekea juu au chini. Na mwishowe ikatupeperusha juu ya tufani. Nami nilikuwa mgonjwa sana tumboni mwangu tulipotua!

211 Baadhi ya hao wahudumu, wahudumu Wapentekoste, wakaingia kwenye motokaa nao walikuwa wakinipeleka Pretoria. Nilitoka Rhodesia ya Kusini; nami nilifika chini kule na nilikuwa mgonjwa, haidhuru. Naye Ndugu Baxter aliketi pale, mgonjwa, na Billy Paul, mgonjwa. Na hapa tulikuwa tukipitia kambini; hapo ndipo wale watu weusi wanaofanya kitu fulani wapaswa kuacha kabila lao, dhambi fulani ya kikabila, nao wanakuja kule. Nao hawangewaruhusu waingie mjini, kwa hivyo wanaishi tu chini ya madebe au cho chote wawezacho, chafu sana na kadhalika, ni kweli. Nao walienda chini pale, nami nikaona pale, uliosema, "Maili ishirini kwa saa." Na hao walikuwa wakiendesha maili sitini na mitano kwa saa. Hao maskini mama wakongwe wakiondoka pale mbio wakiwashika ghafla watoto wao wachanga, vijitoto, uchi, mle barabarani, na yapata umri wa miaka miwili na kuendelea hata mitano au sita; wakiwanyakua watoto hao, na kupaza sauti. Nusura awaue wanne wao wakati mmoja.

212 Nilimgusa mabegani nikasema, "Wewe! Imekuwaje?" Yeye akagueka, kasema, "Ati nini?"

213 Nikasema, "Nilisema, 'Imekuwaje?' Endesha kitu hicho pole pole!"

Kasema, "Tuna amri kupita pale kwa wakati."

214 Nikasema, "Nakuamuru uisimamishe." Naye alisema . . . Nilisema, "Hauwahurumii watu hao?"

"Watu gani?"

Nilisema, "Hao watoto wachanga pale ambao ulikuwa karibu kuwakanyaga."

Kasema, "Hao ni Makafiri!"

215 Nikasema, "Huna aibu! Unajiita Mkristo?" Nikasema, "Hujui kuwa mama huyo angaliwaza vivyo hivyo kuhusu mwanawe, kama ungemwua, kama vile mama yako angaliwaza habari zako?" Nilisema, "Huenda mama huyu akawa asiye na elimu wala maarifa, lakini upendo wa mama humlilia mwanawe. Haikupasi kufanya jambo kama hilo. Na unajiita mwenyewe. . . " Nikasema, "Ule, ubao ule ulisema 'maili ishirini kwa saa.' Biblia yangu ilisema, 'Mpe Kaisari vilivyo vya Kaisari." Naye akainamisha kichwa chake. Nikasema, "Endesha pole pole kwa mwendo maili ishirini kwa saa na uwatendee watu hao kama kwamba walikuwa ndugu zako." Nilisema, "Huna aibu, kitu kama hicho." Ee, jamani, walipayuka-payuka kama vyura waliopigwa bunduki! Lakini hayakuvua dafu, nilitoa maoni yangu, nilipiga ngumi.

216 Basi tulizunguka pale na watu hao walijua nilikuwa upande wao, kuwaletea U—ujumbe wa Injili. Na Mungu angeingia mle.

217 Na kuwachanganya, na kuwaweka wazungu upande mmoja, na weusi mwingine, na pale weusi hawangewazungumzia hata neno moja, wala cho chote. Roho Mtakatifu angeenda kati yao pale na kuwaleta wagonjwa na wanaougua na viwete, na kuwaponya, na kuwaacha *wao* waketi upande huu katika hali yao ya kuwa chini iliyobuniwa kule. Yaonyesha jinsi Mungu hushughulikia mioyo minyenyekevu!

218 Sasa, huyo ni mtu ambaye hajapokea ujumbe bado na yeye anaandika kitabu hicho.

219 Sasa, nifanyeje? Kitu kile, nifanyeje. . .Ni—nirudi kule? Sasa, kama Mungu ananiita kwa uninjilisti, naam, siwezi kuwa nabii Wake na mwinjilisti wakati ule ule. Una. . .Afisi hizo haziwezi kuchanganyishwa, Mimi—mimi. . .Napigana na upepo. Kama nitakuwa mwinjilisti, itanipasa kuwa mwinjilisti. Kama nitakuwa nabii Wake, nitaenda mlimani mahali fulani na kuishi huko; bila kanisa, bila kusanyiko, hata nisikie toka kwa Bwana: kisha nichape miguu nije nikatabiri, ndiposa nichape miguu nirudi tena. Ona? Mojawapo wa mambo haya, yanafikiriwa katika vitu vitatu, kwangu. Ujumbe umekwisha au yanipasa kufanya mojawapo wa hivi vitu viwili. Sijui la kufanya.

220 Usiku uliopita niliota ndoto, nami niliota kuwa nilikuwa naenda mkutanoni, nami sijapata kuona kundi la watu kama hilo! Walikusanyika kama kwenye uwanja mkubwa wa michezo, umbali nilioweza kuona. Na mtu fulani alinifuata wala si Billy, naye akanipeleka kule chini. Nami nilikuwa chumbani mle, nikiomba, nami nilikuwa nakuja kwa. . .chini ya upako; kama wasemavyo, kuwafahamisha, kufikia ambapo nalisikia ingekuwa upambanuzi. Na tulipokuwa tukienda kule chini mtu fulani alianza kuongea nami na, alipofanya hivyo, ule upambanuzi uliniondoka. Singeusikia. Na ndipo nilijaribu

kujiingiza kwake tena; singeweza kufanya hivyo. Singeweza kufanya hivyo kamwe. Kisha nikachoka.

221 Basi nikaanza kutazama kundi lile lilipokuwa likija. Na nilipofanya hivyo, nikasema, "Vema, nina somo niani mwangu ninalojua kuwa madhehebu hayo na jinsi walivyowafanyia watu wale, halafu nitawahubiria Injili hiyo hivyo kwao kwa nguvu niwezavyo." Na nilipoenda jukwaani, hilo likaniacha.

222 Hakuna upambanuzi, hakuna hata moja ya jumbe hizo; nami nikasimama pale, huku watu wanangoja. Nami nikasema, "Nifanyeje?"

223 Na kitu fulani kikasema, "Endelea tu. Endelea tu, ona?" Utatolewa nifikapo kule. "Endelea kusonga mbele." Ona? Ndipo nilikuwa papo napo juk-. . . kisha nikaamka.

224 Huenda ikawa kwa sababu nilikuwa nikiwaza hayo, niliota ndoto kama hiyo. Huenda ikawa hivyo. Huenda ikawa ndoto hiyo ni ya kiroho. Sijui. Sina tafsiri yake, si—sijui maana yake. Siwezi kuwaambia nami—sijui ni nini. Lakini, vyo vyote ilivyo, niko kwenye njia panda mahali fulani. Ona? Kuna kitu fulani, kitu fulani mahali fulani.

225 Nami na—naweza kusema kitu kimoja, nami nafahamika kwa kosa sana. Au tuseme *hivi*, ni. . .ni *hivi*, au *hivyo*, mtu mwingine huipata upande *huu* mbali sana. Na jinsi ilivyo, unasema kitu fulani vema moja kwa moja kutilia mkazo, na mtu mmoja anaielewa *hivi*, kwa hivyo yeye anamwambia mwingine na anaegemea mbali kidogo, na anayefuata anaegemea mbali kidogo, anayefuata anaegemea mbali kidogo, kisha linaenda mbali kabisa. Mmoja analisikia *hivi* yeye anaenda hivi, hivyo, na hivyo. Ona, na unaenda mbali. Na hivyo ndivyo ilivyo kule katika—katika mikutano, na kadhalika, unapoelekea moja kwa moja kwenye Jambo fulani. Sasa, Wateule wangesikia Jambo hilo. Wanatambua Jambo lile! Wanajua, kwa sababu nilisema jinsi hasa ilivyokusudiwa (ona) hivyo, Ujumbe tu, vivyo hivyo.

226 Sasa, na hivyo ndivyo ninavyosema, inaonekana kama kwamba kuna kukosa kufahamu kwingi wakati wote, daima. Ni nini? Ni. . .Nimepanda Mbegu zote zilizohitajika kupandwa? Je, wakati umefika? Je, mjumbe huyu mkuu anajitayarisha kuingia jukwaani hivi sasa? Je, kuja kwa Bwana kumekaribia? Je, ni kuitwa toka kwa nchi hii hadi nyingine? Je, Yeye ameniita kutoka uinjilisti?

227 Kumbuka nina. . .niliyakariri kwa mke wangu. Wengi wenu katika kitabu. . .Siku niliyoweka lile jiwe la pembeni pale, yapata miaka thelathini iliyopita, papo hapo pembeni, yalisema mle. . .Ile asubuhi Yeye aliponiamsha, na nilikuwa nimeketi chumbani mle, hata kabla sijaoa wala lo lote, mhubiri kijana, tu, Yeye alisema, "Fanya *kazi* ya muhubiri wa Injili. Si. . .Wewe si muhubiri wa Injili, lakini fanya kazi ya yake," akaninukuulia Andiko hilo. Nilipokimbia kule chini na kuona hiyo miti miwili,

nikavunjia mmoja *hapa*. . .umoja na utatu. Sikuipitanisha, niliipanda hivyo. Ndipo Yeye aliona tunda likianguka mkononi mwangu kisha akanipeleka upesi hata Kalvari. Sasa, sikiza, Yeye alisema, "Utakapotoka kwa hili, soma 2 Timotheo 4, 2 Timotheo 4."

228 Na iliniacha nimeketi mle chumbani. Hata sikujua ilikuwa ono. Sikujua jinsi ya kuliita wakati huo. Nilikuwa ninaweka jiwe la pembeni (siku hiyo) la msingi pale. Imeandikwa, imewekwa papo hapo pembeni mle sasa, kasema:

> *. . .fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza huduma yako.*
>
> *Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia*. . .kufundishwa —*waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti;*
>
> *. . .na watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo*. (Hao ni wote wale wa umoja na utatu, wamekosa lile . . .)

229 Sasa, Yeye hakusema kamwe "Wewe u mwinjilisti," Yeye alisema, "Fanya kazi yake." Ona? Sasa, je, wakati umefika? Je, nitaendelea mbele na hayo au wakati umekuja wa jambo jingine? Hilo sijui.

230 Na hilo ndilo nililotaka, maongeo ya moyo kwa moyo pamoja nanyi. Basi nimepitisha wakati wangu hivi sasa, wa kuwaruhusu muende, niradhini kwa kuwakawisha sana hivi.

231 Lakini Bwana akipenda, kabla tu Ndugu Boze hajakuja Jumapili, huenda nikaja Jumapili asubuhi na huenda nikahubiri ujumbe uitwao *Ule Uinjilisti wa wakati wa Jioni,* au kitu kama hicho, ona, kama ukipenda, mchungaji. [Ndugu Neville asema, "Sawa! Mungu asifiwe!" Mh.] Bwana akipenda, Jumapili ijayo asubuhi. Nami ningenena kuhusu hayo usiku, nami ningekuwa na maongeo ya moyo kwa moyo labda wakati mwingine, lakini najisikia kama ingekuwa heri hivi, labda, ona, kama hayo ni mapenzi ya Bwana.

232 Natawaombeeni. Niombeeni. Msi—msiseme tu, "Ndugu Branham, nitafanya hivyo." Fanyeni hivyo! Ona? Nategemea hayo. Mimi ndimi ninayehitaji maombi, kama Yeye aweza kunisukumia mahali fulani. Kumbukeni, mimi ni mwanadamu, mimi si Mungu. Mimi ni mwanadamu kama mlivyo ninyi, nikijaribu kupata mapenzi ya Mungu ili nienende kwayo. Hakuna ye yote awezaye kujua hata. . . "Na yeye anayepungukiwa na hekima na aombe dua kwa Mungu." Na hilo ndilo nitakalofanya, kumwomba Mungu. Nami naliweka tu hilo kwenu kama kanisa langu, maongeo ya moyo kwa moyo. Basi, tuko wapi? Tumesimama wapi? Tuko tunaishi kwa saa ipi? Tuko katika wakati wa mwisho, naamini. Naamini tuko mwishoni kabisa.

233 Sasa, inaweza kugeuka upande mmoja au mwingine. Kwa hivyo ninyi. . .Basi au kazi yangu imekwisha, au ninaitwa kwa ajili ya huduma ya nchi za ng'ambo, au Yeye atanifanya mwinjilisti au nabii. Mojawapo wa mambo hayo yapasa kutendeka, kwa sababu mimi niko mwishoni. Sijui la kufanya. Sijui niende wapi. Hata mikutano hii, ninayoifikia, nimekuwa nikiomba, nilisema, "Bwana, sitafanya kama vile nimekuwa nikifanya. Nitaiendea kama tu vile nilivyofanya nyuma kule, nitarudia tena uinjilisti huo hata Wewe unipe wito wa yale yanayonipasa kufanya."

234 Sasa, nimepanda mbegu kila mahali, kanda zimeenda ulimwenguni kote, jumbe zangu zimezunguka ulimwenguni, makanisa yote yanajua habari zake, kila mahali, na wale Baba amewateua atawaita. Ona?

235 Na Sasa inaonekana kama inakuwa kikwazo kwao. Ee, hawautaki kamwe. Sivyo, bwana. Je, nisonge mbele nikawaombee wagonjwa, na ujumbe mdogo rahisi juu ya hayo, ha—halafu nione jinsi Roho Mtakatifu anavyoniongoza? Hilo ndilo ninalotaka kufanya hata atakaponipa wito mwingine. Kwa sababu mtu hajui la kufanya hata ujue toka kwa Mungu ufanye nini, hata utakapojua uelekee wapi.

236 Nami—sitaki kukaa nyumbani mwangu. Ujumbe huu uko moyoni mwangu. Watu wanakufa, wanaanguka, wanaingia Utukufuni. Nifanyeje? Hebu niutangaze kila mahali niwezapo, na kunena habari za Bwana Yesu hata Yeye atakapogeuza mambo. Niombeeni, nitawaombea. Natumai mtafanya hilo.

237 Sasa, kumbukeni Jumatano usiku, mkutano wa maombi, na Ijumaa usiku, mkutano wa wanaume. Je, utakuwako? Huenda nikashuka kuwaona ninyi nyote, niliwaambia ningekuja na kuwaona Ijumaa usiku. Vema, kisha Jumapili asubuhi, Bwana akipenda, nitanena kuhusu *Uinjilisti wa wakati wa Jioni,* Bwana akipenda; huenda nikaugeuza, sijui. Lakini hilo ndilo ninalowazia sasa hivi, aina ya uinjilisti utakaokuwako wakati wa jioni. Kisha Jumapili usiku, sinema ya Ndugu Boze, basi kumbukeni hayo sasa. Naam, tuombeeni, maana juma lijalo tutaingilia shamba la mavuno, Bwana akipenda.

Wampenda? Amina!
Utamtumikia? Amina!
Utamwamini? Amina!
Amina, Amina!

Yu Baba. Amina!
Yu Mwana Amina!
Yu Roho Mtakatifu. Amina!
Amina, Amina!

Tungali tunaimba, Amina! Amina! Amina!
Amina, Amina!

Wampenda? Amina!
Yuaja? Amina!
U tayari? Amina!
Amina, Amina!

Ikiwa usiku huu, u tayari? Amina!
Asubuhi, u tayari? Amina!
Wakati wo wote, u tayari? Amina!
Amina, Amina!

Tungali tukiimba. Amina!
Na kupiga shangwe. Amina!
Na kuomba. Amina!
Amina, Amina!

Njoo Bwana Yesu. Amina!
Tayarisha Kanisa Lako. Amina!
Tunajitayarisha. Amina!
Amina, Amina!

Nataka kuona mama yangu. Amina!
Nataka kuona baba yangu. Amina!
Nataka kumwona Mwokozi wangu. Amina!
Amina, Amina!

Ee, wampenda? Amina!
Utamtumikia? Amina!
Wampenda? Amina!
Amina, Amina!

238 Baba yetu uliye Mbinguni, huu ni...wimbo mdogo wa *Amina*. Twayapenda mafundisho yako, sisi sote twasema Amina! Twampenda Roho, "Amina!" Twaamini Yeye yuaja, "Amina!" Kila Neno unalosema katika Biblia Yako, Bwana, tunaliitikia kwa "Amina!" Twaamini kila Neno, kulifundisha tu vema tujuavyo, jinsi lilivyoandikwa, kila alama, kila kistari kila kitu, kila koma, jinsi tu limeandikwa, kwa kadiri tujuavyo.

239 Ewe Mungu, turudishie sisi, Bwana. Tupee utoshelevu mkuu tunaotarajia, ili sisi siku moja tusikie kupaze sauti kwa Malaika wanapopaza sauti katika pambio za Haleluya angani, kisha Yesu ataonekana kule ng'ambo kisha kanisa litanyakuliwa.

240 Wasioamini watashangaa, "Nini kilitendeka, imekuwaje kwa watu hawa? Walienda wapi?" Ewe Mungu, hawatafahamu, hata hawatamwona. Lakini kanisa litamwona, hao ni walioitwa hao wateule, waliozaliwa mara ya pili, watatoweka tu. Hawatajua hao waliko, watajua tu hawapo: watakuwa pamoja na Bwana wao.

241 Ndipo wakati huo, Bwana, si litakuwa jambo la kuogofya kuachwa hapa, tukijua kuwa wakati wa wokovu umepita? Hamna ukombozi tena! Maandiko yalisema, "Na mwenye uchafu azidi kuwa mchafu, naye mtakatifu azidi kutakaswa." Ee, itakuwa saa ya jinsi gani!

242 Na tujitayarishe sasa, Bwana. Utakuwa wakati wa ajabu vipi iwapo tutajitayarisha tu kukulaki Wewe, Baba, na tukitengeneza mioyo yetu kila siku. Na tukifanya kosa na kuanguka, kama maskini mtu huyu alivyoandika swali hili leo, hebu wajue kuwa Damu ya Yesu Kristo husafisha dhambi zote. Mtu yule hakusudii kufanya hayo, Bwana. Wana njaa na kiu, wakijaribu kurudi katika ushirika huo wa roho. Wainue, Bwana. Wainue juu ya ulimwengu huu wenye giza na unaochukiza, ambapo nuru ya Jua yaweza kuangaza juu ya nafsi zao tena. Wameanguka chini ya—ya—ya upeo mkuu wa—wa mawingu, nao wako chini takatakani, chini katika dhambi hiyo, lakini wakati mmoja waliishi katika ile Nuru ya Jua. Wao—wao wanataka kurudi tena, Bwana. Warudishe usiku huu, Bwana. Na kama kunao wengine hapa ambao hawajawahi kushuhudia kuwa juu pale, na wanajua ya kwamba . . .

243 Haya makombora hapa, na kila kitu kiko tu kulingana na Neno lako, jinsi tu mambo yanavyohitajika kutendeka. Nasi twaona kanisa la ulimwengu jinsi wamefanya. Sisi—sisi twaona tu—tu kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kama tu ilivyokuwa katika siku za Sodoma, jinsi hasa Yesu alisema itakuwa; mawimbi ya maji; jinsi wanawake wangetembea na kuvalia, na jinsi wangekuwa wanaojiingiza kwa mambo yasiyowahusu, na—na watembee wafanyavyo, na hatua za madaha na kuyumba-yumba, na hawajali . . . vivyo hivyo jinsi nabii alivyosema. Jinsi Danieli alivyosema, "Chuma na udongo wa mfinyanzi havingekubaliana." Na, ee, kila kitu, kimetimizwa, Bwana. Tuko katika wakati wa mwisho. Vivuli vinaanguka, Bwana. Ile nuru nyekundu inamulika, kengele zinalia.

244 Ee, Mungu, hebu watu Wako watambue mapema kwamba yule Malaika ataweka mguu Wake juu va nchi na bahari na ainue mikono Yake na kusema, "Hapatakuwa na wakati baada ya haya."

Ndipo Ee, kulia na kuomboleza jinsi gani,
Waliopotea watakapoambiwa yanayowangoja;
Watalilia miamba na milima,
Wataomba, lakini maombi yao yamechelewa sana.

245 Hii ndiyo siku ya wokovu. "Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo roho ayaambia makanisa." Tujalie, Bwana.

246 Na kusiweko na mtu ye yote hapa asiyekuwepo siku hiyo ya Kunyakuliwa. Na tujazwe na upendo wa Mungu na Roho wa Mungu hata Roho Mtakatifu atatunyakua tukali tukingoja, au hata kama tutastarehe katika kura yetu. Kama ulivyomwambia Danieli, "Enenda Zako, Danieli, maana wewe utastarehe. Bali siku hiyo utasimama katika kura yako."

247 Ee Mungu, wewe ulisema, "Hao waongozao wengi ku- . . . toka dhambini kutenda haki watang'aa kuliko nyota milele na

milele." Ni siku ya jinsi gani! Lakini hao waovu watatupwa katika maangamizi. Ee Mungu, fanya watu watambue mahali pao sasa hivi maishani, wapate kumgeukia Yule mwenye Haki kabla hakujachelewa sana milele. Tujalie, Baba.

248 Sasa hali vichwa vyetu vimeinamishwa kwa muda mchache, maombi ya mwisho, je, kuna mmoja anayetaka akumbukwe, akisema, "Ndugu Branham, nauinua mkono wangu, si kwako bali kwa Mungu. Mungu anirehemu na nitakuwepo siku hiyo, nimesafishwa kwa Damu ya Mwana-Kondoo?" Mungu akubariki wewe. Mungu akubariki wewe, wewe, wewe, wewe, wewe, mikono mingi.

249 Sasa, Baba wa Mbinguni, Mungu, bariki kila, kila mmoja. Umeona mikono yao. Unajua mioyo yao.

250 Nasi twatambua, Bwana, kuwa sisi. . .jambo fulani linakaribia kutendeka. Ulimwengu unajua hivyo, wanaimba nyimbo, na televisheni inavumisha mizaha ya fadhaa pamoja na nyimbo. Wanafanyaje? Kama mvulana mdogo anayepiga mbinja gizani, akipitia karibu na makaburi, anaogopa hata kufa, akijaribu kutuliza nerva zake kwa kupiga mbinja. Yeye anajipumbaza tu mwenyewe. Vivyo hivyo taifa hili linacheka tu, kufanya mzaha, . . .? . . . ! Kama tu ilivyosemwa kuwa wakati unakuja ambapo wangefanya hivyo, "Kukataa yaliyo Kweli na kuzigeukia hadithi za uongo," na jinsi "katika siku za mwisho kungetokea wenye kudhihaki na wanaochekelea," na jinsi mambo haya yangekuwa wakati wa mwisho, "wakaidi, wenye kujivuna, wenye mfano wa utauwa, wakiacha ile Kweli," nasi tunaona hayo sasa hivi.

251 Ee Mungu, waamshe watu! Hebu watambue kuwa wanaweza kuhakikishiwa sasa hivi kuwa wamepita toka mautini na kuingia Uzimani. Tunapompokea Kristo, yule Roho Mtakatifu, tunainuka tu juu ya ulimwengu. Ndipo tunajua tumekwisha fufuka pamoja na Yeye, nasi tunangoja tu kule kugeuzwa ambapo mauti itakoma na vitu vinavyokuta (hili gurudumu ndogo la maisha linalofingirika katika hisi zetu) vitakombolewa. Ee Mungu! Ndiposa tutakuwa na mwili kama Wake na tutaishi Milele pamoja Naye, ile Nchi kuu ya ahadi, tukiwa na ile Bayana.

252 Hebu mtu ye yote asiikose, Bwana. Wale walioinua mikono yao, hebu wakivurumishwe (usiku huu) waingie katika Ufalme ule. Labda waendapo nyumbani, huenda mume akamwambia mke wake, "Mpenzi, kitu fulani kilinigusa usiku huu;" au mke amwambie mumewe, "Mpenzi na—nalijisikia ajabu sana." "Naam, mpenzi, hebu na tupige magoti hapa kando ya kitanda. Hatujafanya hivi hapo mbeleni, lakini hebu na tuombe usiku huu. Hebu tumwombe Mungu aturehemu na atukusanyishe. Nakupenda kipenzi."

253 Na mwi—mwingine, wa kiume amwambie wa kike, na jinsi wanavyopendana, "Ni—ni—ninataka kuwa Mbinguni pamoja nawe. Sitaki kuikosa. Na siku moja tutokapokaribishwa Nyumbani na nitakushika mkono na kutembea kwenye ukumbi mkuu na bustani za Milele, ambapo mwana-kondoo na—na simba watakua pamoja, na mbwa mwitu na ng'ombe watalala pamoja. Na hakutakuwa na kifo wala huzuni tena. Na tutakapotembea kule nyimbo za taifa zitavuma kote hewani, za malaika pambio juu yetu, Malaika watakapotukaribisha sisi Nyumbani, nataka niwe pamoja nawe kule, kipenzi. Ni—ninakupenda wewe," labda unazeeka, "nakumbuka nilipokuoa, maskini uso wako mdogo na mrembo." "Na—nawe, nami nakukumbuka, kipenzi, ulipokuwa kijana mzuri wa umbo."

254 Lakini haya yote yatarudishwa. Yeye aliyeupamba uso wako mrembo wakati mmoja ana m—mchoro wake niani Mwake. Yeye aweza kukupaka rangi tena kule ng'ambo ambako haitafifia tena. Ee Mungu, hebu watu wajue kuwa hii si ndoto ya kubuniwa, lakini ni—ni Kweli, na Mungu, Roho Mtakatifu, yuko hapa kushuhudia. Neno Lake katika nyakati zote limenena kuhusu hayo. Hebu tutazame nyuma na kuona, tukasoma historia yetu. Na mtu ye yote aliyewahi kuwa cho chote duaniani ni mtu, mtu mcha Mungu, hata Marais wetu kama Washington, Lincoln, na wengineo, *akina Yoshua,* na—na . . . *akina Musa,* na wale walio . . . Watu wakuu wa ulimwengu wamekuwa watu walioamini katika hayo, na wametia muhuri ushuhuda wao, nao wanangojea kule ng'ambo ufufuo huo. Tuna malimbuko yake, ile Arabuni.

255 Naomba sasa kuwa kupitia kwa ombi langu Wewe utawapokea watu hawa na maombi yao na kuwaingiza katika huo Ufalme. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

256 Mungu awabariki, awe mwingi wa rehema kwenu, afanye uso wake ung'ae juu yenu, na awalinde na awabariki katika baraka zote za Kimbinguni.

257 Sasa nasema haya, si kwa ukali, bali kwa upendo. Nawasihi ninyi msiomjua Yeye kuwa mito yenu itakuwa migumu sana hata msiweze kulala tena, vyakula vyenu vitakuwa vibaya sana hata msiweze kula tena, hata mwende kando mahali fulani na kusema "Bwana unirehemu mimi." Hiyo si kukutakieni cho chote kibaya. Hiyo ni kwa manufaa yako, ndugu, dada. Naomba tu kuwa itakuwa hivyo kwenu.

Hata twonane huko juu,
Hata twonane Kwake kwema; (Kwake kwema!)
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

Mungu awe nanyi daima
Hata twonane ya pili,
Awapasulie kina,
Mungu awe nanyi daima . . .

258 Sasa kwa ajili wa wakati wa kale, hebu tusalimiane kwa mikono na mtu fulani sasa [Ndugu Branham asalimiana kwa mikono na watu katika beti tatu zinazofuata—Mh.]

Hata twonane huko juu,
Hata twonane Kwake kwema; (Kwake kwema!)
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

Hata twonane huko juu!
Hata twonane Kwake kwema;
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

Hata twonane huko juu!
Hata twonane Kwake kwema;
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

259 Mwakumbuka tulikuwa tukiimba nyimbo hizo? Hebu tu . . . Na huu mwingine tulikuwa tukiuimba, miaka mingi iliyopita, sijui kama kuna ye yote humu au la, tulipokuwa tukishikana mikono kuzunguka jiko kuukuu hapa, na matope sakafuni. Je, mwakumbuka hayo? Tungeimba:

Twenenda Sayuni,
Mji mzuri Sayuni,
Twenenda juu Sayuni,
Ni maskani ya Mungu.

260 Mwajua katika ule Utawala wa Miaka Elfu jinsi Sayuni itakavyokuwa? Kutakuwako na Nuru Sayuni, na itakuwa kwa ajili ya kivuli cha jua wakati wa mchana na kama Nuru usiku, kwa kuwa hakutakuwa na usiku kule. Lo; jamani!

Twaona rohoni
Baraka za Mungu,
Tusijafika Mbinguni
Tusijafika Mbinguni
Kwenye utukufu
Kwenye utukufu.

Sote pamoja sasa,

Twenenda Sayuni
Mji mzuri Sayuni
Twenenda juu Sayuni
Ni maskani ya Mungu

261 Naupenda huo, nafikiri ni mzuri mno. Sasa, si mnapenda hizo nyimbo za kale? Nadhani ni bora kuliko huu upuzi uliobuniwa tulio nao siku hizi unaoitwa nyimbo. Nazipenda tu. Nami nilikuwa naimba wimbo wa kale kanisani, mwakumbuka.

Nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi
Kuna nafasi yako Kisimani.

262 Lo, jamani! Hizo nyimbo nzuri za kale, naamini kalamu ile iliongozwa na Roho Mtakatifu, wale walioandika nyimbo hizo.

Karibu na Wewe
Mungu wangu;
Karibu zaidi,
Bwana wangu;

263 Hata hivyo, Charles Wesley pamoja na hao waandishi mashuhuri walioandika nyimbo hizo hivyo, hao washairi. Ni tamu, nafikiri ni nzuri sana. Ndiposa tulikuwa tuki. . . Kumbukeni hayo:

Nchi nzuri, nchi nzuri,
Nasimama mlimani,
Naona nchi ya mbali Iliyowekwa tayari;
Niitazamie pwani Ya nchi yangu Mbinguni.

264 Mnakumbuka wakati wa kwanza ambapo Malaika alipokuja kule mtoni? Tulikuwa tukiimba:

Ukingoni mwa Yordani
Ninaangalia,
Bara nzuri ya Kanaani
Ninayotamani

Tutakaa pamoja na Yesu
Katika Pwani yenye raha
Tataimba wimbo wa Musa na Kondoo
Milele hata milele.

265 Tulipokuwa tukiimba huo, Sauti ililia toka angani, na hapa kukaja hiyo Nguzo ya Moto ikizunguka-zunguka na kushuka ikisema, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule kuja Kwake kwa kwanza, una Ujumbe utakaotangulia kule kwa Pili." Tazama ulikoenda. Hiyo ni miaka thelathini na mmoja iliyopita. Tazama ulikoenda tokea hapo, kote ulimwenguni katika moto wa mikutano ya ufufuo. Na sasa tunaiona ikipoa. Wakati umekaribia.

266 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tukikumbuka matangazo yote.

267 Mchungaji mkuu wa kondoo, tunayetarajia kuona akija siku moja, mioyo yetu inatarajia saa hiyo tutakapomwona Yeye. Siku moja uliketi juu ya mlima na ukawafundisha watu Wako, ukasema, "Ombeni hivi," [Ndugu Branham na makutano waomba pamoja—Mh.]:

. . .Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe,

Ufalme Wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

Utupe leo riziki yetu.

Na utusamehe makosa yetu kama sisi nasi tusamehevyo wanaotukosea.

Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu; kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, sasa na hata milele. Amina.

268 Biblia ilisema, "Nao waliimba wimbo wakatoka nje."

Peleka Jina la Yesu
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako,

Thamani, na tamu
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani na tamu (na tamu!)
Ni Jina Lake Yesu.

269 Si hilo laonekana tamu? Hebu acha mara moja, mara moja hapa na pale, na uusikize tena tunapouimba.

Katika Jina la Yesu,
Ninamwinamia; (Ona)
Ndiye Mfalme wa Wafalme,
Katika ya maisha.

Lo, si huo ni mtamu? Hebu tuone:

Peleka Jina la Yesu,
Liwe silaha yako;
Utakapojaribiwa,
Lilia tu Jina hilo. (Ona?)

Lo, Jina la dhamani! Hebuni tuuimbe:

Peleka Jina la Yesu,
Liwe silaha yako;
Utakapojaribiwa
Lilia Jina hilo.

Dhamani na tamu (dhamani) Na tamu! (Na tamu)
Ni Jina Lake Yesu.
Dhamani na tamu (na tamu)
Ni Jina Lake Yesu.

270 Sasa, kama tukiinamisha vichwa vyetu, mchungaji wetu ataliruhusu kusanyiko liondoke kwa maombi. Bwana awabariki, Ndugu Neville.

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org